**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

# MKOA WA KIGOMA

## MPANGO MKAKATI

## (MWAKA 2012/13 – 2016/17)

MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
S,L P 332,
KIGOMA, Tanzania.
Simu: +255 028 280 4865,
Faksi: +255 028 280 2719
Baruapepe: kigomadistrictcouncil@yahoo.com
Tovuti:

*Januari 2013*

# Yaliyomo

ORODHA YA VIFUPISHO................................................................................................ ii

DIBAJI.............................................................................................................. vi

MUHTASARI RASMI....................................................................................................... viii

SURA YA KWANZA.............................................................................................. x

1.0 Utangulizi................................................................................................... 1

1.1 Mkabala uliotumika katika kuandaa mpango.................................................... 1

1.2 Madhumuni ya Mpango Mkakati....................................................................... 1

1.3 Historia ya Halmashauri ya Wilaya Kigoma................................................ 2

1.4 Makabila........................................................................................................ 2

1.5 Mageuzi ya Serikali za Mitaa............................................................................ 3

1.6 Taarifa za Msingi za Halmashauri ya Wilaya.................................................... 3

1.6.1 Eneo la Halmashauri ya Wilaya na mipaka yake ………………………3

1.6.2 Eneo na Idadi ya Watu...................................................................................... 3

1.6.3 Muundo wa Uongozi......................................................................................... 4

1.6.4 Hali ya hewa na tabianchi………………………………………………..4

1.7 Kanda za Ikolojia- Kilimo…………………………………………………… 4

1.7.1 Ukanda wa Ufukwe wa Ziwa............................................................................. 4

1.7.2. Msitu wa Miombo................................................................................................ 5

1.7.3 Kanda ya Kati..................................................................................................... 5

1.7.4 Nyanda za Juu Kaskazini..................................................................................... 5

1.7.5 Nyanda za Juu Kusini........................................................................................... 5

1.8 Hali ya Ardhi............................................................................................................ 6

1.9 Sura ya Nchi.............................................................................................................. 6

1.10 Shughuli za Kiuchumi........................................................................................... 6

SURA YA PILI.......................................................................................................... 1

UCHANGANUZI WA HALI......................................................................................................... 7

2.0 Utangulizi......................................................................................................... 7

2.1 Upitiaji tena wa Utoaji wa Huduma za Kijamii na Kiuchumi.......................................7

2.1.1 Utoaji wa Huduma za Kijamii.................................................................................... 7

2.1.1.1 Elimu......................................................................................................... 8

2.1.1.2 Afya......................................................................................................... 9

2.1.1.3 Maji......................................................................................................... 10

2.1.2 Utoaji wa Huduma za Kiuchumi......................................................................... 10

2.1.2.1 Kilimo......................................................................................................... 10

2.1.2.2 Mifugo......................................................................................................... 11

2.1.2.3 Vyama vya Ushirika……………………………………………………… 12

2.1.2.4 Ujenzi......................................................................................................... 12

2.1.2.5 Maendeleo ya Jamii......................................................................................... 12

2.1.2.6 Maliasili......................................................................................................... 13

2.1.2.7 Ardhi......................................................................................................... 14

2.1.2.8 Utawala na Utumishi......................................................................................... 14

2.1.2.9 Mipango......................................................................................................... 15

2.1.2.10 Fedha na Biashara......................................................................................... 15

2.1.2.11 Ukaguzi wa Hesabu wa Ndani......................................................................................... 15

2.1.2.12 Masuala ya Kisheria.........................................................................................15

2.1.2.13 Kitengo cha Kusimamia Ununuzi......................................................................................... 16

2.1.2.14 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)............................................... 16

2.1.2.15 Masuala Mtambuko......................................................................................... 16

2.2 Raslimali Kuu zilizopo......................................................................................... 18

2.2.1 Ardhi......................................................................................................... 18

2.2.2 Misitu:......................................................................................................... 18

2.2.3 Winyama pori:......................................................................................................... 18

2.2.4 Ugugaji Nyuki........................................................................................................19

2.2.5 Uvuvi..................................................................................................................... 19

2.2.6 Utalii:.................................................................................................................... 20

2.2.7 Madini.................................................................................................................. 21

2.3 Uchanganuzi wa Wadau............................................................................................ 7

Jedwali 2.3.1 Uchanganuzi wa Wadau...................................................................22

2.4Uchanganuzi wa SAOC......................................................................................... 22

SURA YA TATU.........................................................................................................

DIRA, DHAMIRA, MALENGO NA MAADILI YA MSINGI........................................... 36

3.0 Utangulizi............................................................................................................... 36

3.1. Dira...................................................................................................................... 36

3.2 Dhamira................................................................................................................. 36

3.3 Maadili Makuu........................................................................................................ 36

3.4 Maeneo ya Matokeo Muhimu (KRAs)........................................................................ 37

3.5 Malengo ya Pamoja.................................................................................................. 40

SURA YA NNE...........................................................................................................

MALENGO MKAKATI, SHABAHA NA MIKAKATI.............................................................. 41

4.0 Utangulizi…………………………………………………………………… 41

4.1 IDARA: MIPANGO.................................................................................................. 41

4.2 IDARA: MAENDELEO YA JAMII.............................................................................. 43

4.3 IDARA: AFYA......................................................................................................... 47

4.4 IDARA: ELIMU YA SEKONDARI.............................................................................. 56

4.5 IDARA: MAJI.......................................................................................................... 63

4.6 SEHEMU: TEHAMA................................................................................................ 66

4.7 SEHEMU: SHERIA.................................................................................................. 67

4.8 IDARA: UJENZI...................................................................................................... 69

4.9 IDARA: ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA.............................................................. 73

4.10 IDARA: BIASHARA NA FEDHA........................................................................... 74

4.11 SEHEMU: KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI......................77

4.12 SEHEMU: KITENGO CHA UNUNUZI (PMU)..................................... 79

4.13 IDARA: KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA........................................... 81

4.14 SEHEMU: MIFUGO NA UVUVI........................................................................ 88

4.15 IDARA: USAFI NA MAZINGIRA........................................................................... 96

4.16 IDARA: ELIMU YA MSINGI.................................................................................. 97

4.17 IDARA: UTAWALA.................................................................................................. 103

4.18 SEHEMU: UCHAGUZI........................................................................................... 108

SURA YA TANO..................................................................................................................

UFUATILIAJI NA TATHMINI.............................................................................................

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CAG | - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali |
| DALDO | - Ofisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo wa Wilaya |
| DCDO | - Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya |
| DCO | - Kitengo cha Ushirika cha Wilaya |
| DE | - Mhandisi wa Wilaya |
| DED | -Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya |
| DEO (P) | - Ofisa Elimu wa Wilaya (Msingi) |
| DEO (S) | -Ofisa Elimu wa Wilaya (Sekondari) |
| DFsOQ | -Ofisa Mdhibiti wa Ubora wa Uvuvi |
| DFsOAQ | - Ofisa wa Ufugaji Samaki wa Wilaya |
| DIA | -Mkaguzi Hesabu wa Ndani |
| DLaDO | -Ofisa Uendelezaji Ardhi wa Wilaya |
| DMO | -Daktari wa Wilaya |
| DSMS –IRR | -Mtaalamu wa Umwagiliaji wa Wilaya |
| DSMS – PP | -Mtaalamu wa Kuhifadhi Mimea wa Wilaya |
| DSMS – CI | -Mtaalamu wa Kukagua Mazao wa Wilaya |
| DSMS – CP | -Mtaalamu wa Uzalishaji Mazao wa Wilaya |
| DSMS – HORT | -Mtaalamu Kilimo cha Mazao ya Bustani wa Wilaya |
| DSMS – LUP | -Mtaalamu wa Mipango ya Utumiaji Ardhi |
| DSMFSS | -Mtaalamu wa Takwimu za Uvuvi wa Wilaya |
| DNRO | -Ofisa Maliasili wa Wilaya |
| DPLO | -Ofisa Mipango wa Wilaya |
| DT | -Mweka hazina wa Wilaya |
| DVO | -Ofisa Mifugo wa Wilaya |

| | |
|---|---|
| DWE | -Mhandisi wa Maji |
| FsO | -Ofisa Uvuvi |
| HBFS | -Mfumo wa Mfuko wa Pamoja wa Afya |
| HIV/AIDS | -Virusi vya UKIMWI/Upungufu wa Kinga Mwilini |
| IEC | -Utoaji wa Taarifa za Elimu |
| KDC | -Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma |
| LGAs | -Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| LGCDG | -Ruzuku ya Mtaji wa Maendeleo ya Serikali za Mitaa |
| LO | -Mwanasheria |
| MTEF | -Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati |
| PMO-RALG | -Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PMU | -Kitengo cha Kusimamia Ununuzi |
| PPA | -Sheria ya Ununuzi wa Umma |
| PPR | -Kanuni ya Ununuzi wa Umma |
| RM | -Usimamizi wa Masafa (Range Management) |
| SA | -Wanyama Wadogo |
| SACCOS | -Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa |
| SP | -Mpango Mkakati |
| TACAIDS | -Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania |
| TANROAD | -Mamlaka ya Barabara Tanzania |
| VPH | -Afya ya Mifugo (Veterinary Public Health) |
| WDC | -Kamati ya Maendeleo ya Kata |

**DIBAJI**

Mpango Mkakati huu wa miaka mitano kuanzia kipindi cha 2012/2013 hadi 2016/2017 unalenga kutekeleza Dira na Dhamira ya Baraza ili kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa watu wa wilaya ya Kigoma ambavyo vitachapuza ukuaji wa uchumi na kufikia maendelao endelevu.

Mpango unasisitiza kuboresha uzalishaji kupitia mikabala mingi kama vile kuimarisha huduma za ugani, miundombinu, vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) pamoja na kuwaendeleza wanawake na vijana katika shughuli za kuongeza kipato. Shughuli hizo zinatarajiwa kusaidia kuongeza uzalishaji. Baraza limechukua hatua zinazofaa katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaweza kutokea.

Maeneo mengine ya kupewa kipaumbele katika kipindi cha mpango mkakati yanajumuisha Usimamizi wa Fedha na Uwajibikaji, Uendelezaji wa Raslimali Watu na Utoaji wa Huduma Bora za Jamii. Hata hivyo, Utawala Bora unachukuliwa kuwa kipengele muhimu katika kudumisha amani na usalama kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Zaidi ya hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma itaweka juhudi maalumu katika kutekeleza masuala mtambuko ya mazingira, jinsia na VVU/UKIMWI kwa kuhamasisha jamii, kujenga utambuzi na mazingira yanayofaa kwa ajili ya wanawake na vikundi vya watu walio katika mazingira magumu. Mara kwa mara Halmashauri imekuwa ikipata msaada wa Ruzuku ya Mtaji wa Maendeleo wa Serikali za Mitaa (LGCDG) na Mfumo wa Mfuko wa Pamoja wa Afya (HBFS) katika kutekeleza kazi zake nyingi.

Kuhusiana na janga la VVU/UKIMWI, kuna juhudi zinazoendelea zinazofanywa na Halmashauri za kuinua utambuzi wa jamii kuhusu vyanzo, uambukizaji na mbinu za uzuiaji. Hatua mahsusi zinazochukuliwa zinajumuisha utoaji habari kwa umma, Elimu na Mawasiliano (IEC) kwa kushirikiana na TACAIDS, Mashirika ya Asasi za Kiraia (CSOs) na wabia wengine wa maendeleo.

Mpango unafafanua masuala kadhaa muhimu kuanzia uchanganuzi wa hali ya wilaya, dira na dhamira. Unafafanua pia malengo ya Halmashauri, shabaha na uwekaji wa mikakati ili kufikia shabaha na malengo yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, viashirio vya utendaji vimebainishwa ambavyo vitaiwezesha Halmashauri kupima ufikiaji wa shabaha na malengo.

Katika baadhi ya sehemu za mpango huu, data husika zimetolewa katika kuelezea hali ya sasa ya huduma na maelezo mafupi ya Halmashauri.

Mwisho Halmashauri inapenda kuwashukuru wote waliohusika katika kuandaa Mpango Mkakati huu. Shukrani za pekee zinatolewa kwa wafuatao: Madiwani, Maofisa Watendaji wa Kata na vijiji, Makatibu Tarafa, Viongozi wa Vyama wa Siasa, Viongozi wa Dini, na Mashirika ya Asasi za Kiraia. Aidha, Halmashauri inatoa shukrani zake kwa wataalamu wote wa Halmashauri kwa kujitoa kwao na mchango wao katika kuandaa Mpango Mkakati huu.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninamshukuru Bw. Mofulu George na Bibi Devotha Joseph wa Kampuni ya EDENCONSULT kwa kuwezesha maandalizi ya Mpango Mkakati huu. Ni matumaini yangu kuwa Mpango Mkakati wa 2012/2013 - 2016/2017 utaleta mafanikio yanayofaa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika Halmashauri yetu.



Saini............................ Tarehe...........................

HAMIS S. BETETSE

MWENYEKITI

**HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA**

## MUHTASARI RASMI

Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma unahusu kipindi cha miaka mitano kuanzia 2012/2013 hadi 2016/2017. Utayarishaji wake uliongozwa na sera mbalimbali na kanuni za kitaifa pamoja na mikakati ya kisekta. Hususan, Mkakati wa Taifa wa Ukuaji wa Uchumi na Upunguzaji wa Umaskini (MKUKUTA 11), Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2011-2015), Dira ya 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na sera za sekta nyingine vimeongoza utayarishaji wa Mpango Mkakati huu. Zaidi ya hayo, mabadiliko na mageuzi ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea yamezingatiwa katika utayarishaji wa Mpango Mkakati huu.

Uundaji wa dira, dhamira ma maadili ya msingi pamoja na ubainishaji wa malengo, shabaha na mikakati ulifanywa kupitia warsha ya wadau. Dira ya Halmashauri ya wilaya inasema kwamba *"**Halmashauri ya wilaya inaazimia kuwapatia wakazi wake maendeleo endelevu pamoja na miundombinu iliyoboreka, mawasiliano na upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi ifikapo 2025".***

Wakati dhamira yake inasema kuwa, **" *Kuimarisha uwezo wake yenyewe na ule wa taasisi za kijamii ili kuweza kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi na miundombinu inayofaa kwa kushirikiana na wabia wengine wa maendeleo ndani ya vigezo vya utawala bora".***

Mpango Mkakati huu umegawanywa katika sura tano, ambapo sura ya kwanza inaelezea mtazamo wa jumla wa mkabala uliotumika katika kutengeneza waraka huu wa mpango mkakati, malengo ya mkakati, mageuzi ya serikali za mitaa na muhtasari wa uchumi na jamii wa Wilaya. Sura ya pili inatoa uchanganuzi wa hali na mtazamo wa kina wa utoaji huduma za kijamii na kiuchumi wa sekta mbalimbali. Zaidi ya hayo, uchanganuzi wa SAOC na wadau umechukuliwa kama sehemu ya uchanganuzi wa hali. Sura ya tatu inawasilisha Dira, Dhamira, Maadili ya Msingi na malengo mkakati ya Halmashauri pamoja na Maeneo Muhimu ya Matokeo (KRAs).

Katika sura ya nne mpango unaelezea malengo na mikakati ambayo imetokana na malengo mkakati yaliyokubaliwa. Aidha, unaonyesha viashio vikuu vya utendaji (KPIs), njia za uthibitishaji na mtu anayehusika na kila lengo. Sura ya mwisho inaelezea jinsi ufuatiliaji wa mpango utakavyofanyika pamoja na tathmini ya utendaji katika ngazi tofauti na katika vipindi tofauti.

Katika kuhitimisha, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika kutayarisha Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwa mwaka 2012/2013-2016/2017. Ni imani yangu kwamba, Halmashauri itaendelea kutenda kazi zake vizuri kwa viwango vya hali ya juu na kuendeleza maadili yake ya msingi huku ikifuata kanuni za Utawala Bora.



Saini.................................... Tarehe......................

MIRIAM P. MMBAGA

MKURUGENZI MTENDAJI

**HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma unajumuisha kipindi cha miaka mitano kuanzia 2012/13 hadi 2016/17. Mpango unafafanua Dira yetu, Dhamira, Maadili ya Msingi, Malengo, Shabaha na Viashirio Vikuu vya Utendaji. Zaidi ya hayo, unatoa taratibu za ufuatiliaji na tathmini zitakazotumiwa ndani ya mpango huu.

Kwa kuzingatia mamlaka yake ya kawaida na mamlaka ya kisheria, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inahitajika kutoa huduma kwa wakazi wa Wilaya ya Kigoma kwa namna inayofaa na yenye ufanisi na kuendeleza ushirikiano na vikundi vya kiraia na watu wengine au mamlaka kama ilivyotajwa kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa [SURA 288 Iliyorekebishwa 2002].

## 1.1 Mkabala Uliotumika katika Kutayarisha Mpango Mkakati

Utayarishaji wa Mpango Mkakati huu ni kwa mujibu wa masharti ya Sheria Namba 9 ya 1982 ambayo inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutayarisha Mipango Mkakati ya miaka mitano itakayotumika kama miongozo katika kutayarisha mipango na bajeti za MTEF. Mpango Mkakati huu unabainisha maeneo ya vipaumbele ya utoaji wa huduma na kazi nyingine za kawaida zitakazofanywa na Halmashauri.

## 1.2 Madhumuni ya Mpango Mkakati

Mpango Mkakati uliotayarishwa utatumika kama Chombo cha kutekelezea dira, dhamira, malengo na hatua za zitakazochukuliwa kwa miaka mitano. Madhumuni ya Mpango Mkakati huu ni;

- Kushughulikia masuala muhimu ili kuweka jitihada za kuboresha utendaji.
- Kuhakikisha kuwa kuna uratibu pamoja na wadau wengine ili kuhimiza utumiaji wa juhudi, akili za watu na maliasili za ndani na za taifa ili kufikia malengo ya maendeleo yaliyopangwa.
- Kuhakikisha kuwa wadau wote (umma na binafsi) wanashirikishwa kikamilifu katika kufanikisha dira na dhamira ya Halmashauri.

- Kuhakikisha kuwa vipaumbele vya jamii vilivyobainishwa vinatekelezwa na wadau wote katika Halmashauri ya Wilaya.
- Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa malengo mkakati yaliyowekwa.
- Kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu wa kufuatilia na kutathmini miradi ya utawala bora.

### 1.3 Historia ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ilianzishwa mnamo Julai, 1984 kwa masharti ya sehemu ya 8 na 9 ya Sheria ya Serikali za Mitaa 1982 (Mamlaka za Wilaya) na Madiwani 32, ambapo miongoni mwao 25 walichaguliwa kutoka katika Kata ndani ya Halmashauri (mmoja kutoka katika kila Kata), 7 walichaguliwa na Halmashauri kutokana na watu walioteuliwa na jumuiya za chama.

### 1.4 Makabila

Makabila yaliyopo katika Wilaya hii yanajumuisha: Waha, Wabembe, Wabwari, na Watongwe. Waha ni asilimia 95 ya idadi ya watu na wanaishi katika maeneo yenye msongamano mkubwa ya Uvinza.

Kwa kuwa lengo kuu la Halmashauri ni kutoa huduma kwa watu wake kwa hiyo, inakusudia kutoa huduma bora zaidi na endelevu kwa watu kwa kufikia malengo yafuatayo:

- ❖ Kuhakikisha watu wake wanaishi viwango bora vya maisha.
- ❖ Kuhakikisha kuna utawala bora.
- ❖ Kutoa elimu kwa watu wake.
- ❖ Uchumi wa ushindani.

Ili kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zimepitia hatua kadhaa katika Mageuzi ya Serikali za Mitaa kama sehemu ya mchakato wa Ugatuaji Madaraka.

## 1.5 Mageuzi ya Serikali za Mitaa

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni miongoni mwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilihusika katika programu ya Mageuzi ya Serikali za Mitaa yaliyoanza mwaka 1999. Lengo kuu la mageuzi ya Serikali za Mitaa ni kujenga uwezo; Yafuatayo yamezingatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

- Mageuzi ya mtazamo wa muundo wa Halmashauri
- Utawala
- Usimamiaji wa huduma za umma
- Mageuzi ya Fedha ya Serikali za Mitaa n.k.

## 1.6 Taarifa za Msingi za Halmashauri ya Wilaya

Sehemu hii inatoa taarifa za msingi za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ikiwa ni pamoja na mahali, eneo lake na idadi ya watu, hali ya hewa, tabia nchi, maeneo ya ikolojia ya kilimo na shughuli kuu za kiuchumi. Zaidi ya hayo, inaelezea pia sura ya nchi, hali ya ardhi na mfumo wa utawala.

### 1.6.1 Eneo la Halmashauri ya Wilaya na mipaka yake.

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iko kati ya latitudo $4^{0}45^{'}$ hadi $6^{0}30'$ K na longitudo 29045'hadi $31^{0}30'$ MS. Kwa upande wa Kaskazini wilaya inapakana na wilaya ya Kasulu, upande wa Mashariki inapakana na mkoa wa Tabora/Katavi (wilaya ya Urambo), kwa upande wa Kusini mkoa wa Rukwa/Katavi (wilaya ya Mpanda ), na upande wa Magharibi inapakana na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

### 1.6.2 Eneo na Idadi ya Watu

Wilaya ina eneo la jumla ya Kilometa za mraba 19 574 ambazo kati ya hizo Kilometa za mraba 8 029 ziko chini ya maji (hasa Ziwa Tanganyika na maziwa madogo ya Nyamagoma na Sagara) na sehemu iliyobakia ya Kilometa za mraba 11 545 ni nchi kavu.

Ardhi inayolimika inakadiriwa kuwa zaidi ya $Km^2$ 10 150 (hekta 1 015 630) ambapo kati ya hizo ni asilimia 18 tu ndiyo imeendelezwa. Jumla ya eneo linalotumiwa kwa kilimo linakadiriwa kuwa Kilometa za Mraba 1 900 (hekta 182 813.4), Hifadhi ya taifa ya Mahale na Gombe ni Kilometa za Mraba 6 613.354 , mashamba makubwa ya misitu hekta 240.9 na hifadhi ya misitu ya asili inachukua hekta 494 835.4.

Misha ya kaya katika wilaya ya Kigoma kimsingi hutegemea kilimo. Kwa ujumla wilaya inajitegemea kwa mahitaji ya chakula.

Kwa mujibu ya sensa iliyofanyika mwaka 2002, idadi ya watu katika wilaya ilikuwa 480,81 6 (ambapo 253,474 ni wanawake na 237,342 ni wanaume) kuna jumla ya kaya 72,085 na ukubwa wa kaya wa 6.8. Kwa kiwango cha ukuaji cha asilimia 4.1 wilaya inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 718,598 mwaka 2012.

### 1.6.3 Muundo wa Utawala

Kiutawala wilaya imegawanyika katika tarafa sita, ambazo ni Mwandiga, Mahembe, Ilagala, Kalinzi, Buhingu na Nguruka. Aidha, kuna kata ishirini na tano (25), vijiji 78 na vijiji vidogo 471 (Vitongoji). Kitabia nchi wilaya imegawanyika katika maeneo matatu – Nyanda za juu, maeneo ya nyanda za chini, na eneo la misitu la Miombo. Kwa upande mwingine, Ziwa Tanganyika linasababisha mgawanyo mzuri wa mvua.

### 1.6.4 Hali ya hewa na tabia nchi.

Kitabia nchi wilaya imegawanyika katika maeneo matatu ambayo ni nyanda za juu na chini na eneo la misitu ya miombo. Mgawanyo wa mvua ni kati ya mm 600 hadi mm 1600 kwa msimu; na halijoto huanzia nyuzi joto $22^{o} – 32^{o}$. Maeneo yamegawanywa kulingana na aina za udongo, mazao, na kiasi cha mvua.

## 1.7 Kanda za Ikolojia - Kilimo

Wilaya inaweza kugawanyika katika kanda tano za uchumi wa kilimo:

### 1.7.1 Kanda ya Ufukwe wa Ziwa

Ni kipande cha ardhi kati ya milima ya ndani na Ziwa Tanganyika. Iko ndani ya bonde la ufa upande wa magharibi kwa miinuko kuanzia mita 800 – 1,700 kutoka usawa wa bahari. Mvua kwa mwaka zinatofautiana kuanzia milimita 1000 – 1,400 pamoja na kipindi cha ukame cha miezi minne (Juni- Septemba). Ardhi katika eneo la ufukwe wa ziwa ni ndogo, iliyokauka sana, udongo tifutifu wa kahawia wenye mchanganyiko wa nyekundu na nyeusi. Katika ardhi udongo unatofautiana kuanzia udongo wa mfinyanzi mwekundu, nyeusi iliyokolea na rutuba ya wastani. Katika kanda yote uvuvi ulikuwa ni shughuli muhimu ya kiuchumi, lakini sasa

uzalishaji wa mazao unaongoza. Mazao makuu yanayolimwa ni mihogo, mawese, maharage, mahindi na mpunga. Mawese na mpunga hulimwa kwenye mabonde.

### 1.7.2. Msitu ya Miombo

Kanda hii iko kati ya milimita 1,000 – meta 1,200 kutoka usawa wa baharia na mvua kwa mwaka kuanzia milimita 600 – 1,000. Ardhi katika mteremko na miinuko ina kina, udongo wa mfinyanzi uliokauka vizuri hadi udongo mwekundu wa mfinyanzi ulio juu ya udongo mweusi wa mfinyanzi. Mteremko na miinuko ina udongo wa mfinyanzi ambao haujakauka vizuri wa rangi ya kijivu iliyokolea hadi udongo mweusi. Mazao makubwa yanayolimwa ni mpunga, tumbaku, maharage, karanga, mahindi, mihogo, viazi vitamu na mafuta ya mawese. Michikichi na mpunga hulimwa chini ya mabonde. Mifugo mikuu inajumuisha mbuzi, ng'ombe na kuku.

### 1.7.3 Kanda ya Kati

Iko eneo la uwanda wa juu kaskazini lenye watu wengi na lenye msitu ya miombo michache. Mwinuko ni meta 1200 – 1500 kutoka usawa wa bahari na mvua kwa mwaka kuanzia milimita 850 – 1500. Ina mifereji na mito inayopatikana mwaka mzima. Ardhi ni nyeusi yenye wekundu hadi udongo wa mfinyanzi wenye rangi nyekundu iliyokolea ambayo ina rutuba ya wastani. Mazao makuu yanayolimwa ni mahindi, maharage, michikichi, ndizi, tumbaku na matunda kama vile Mananasi.

### 1.7.4 Nyanda za Juu Kaskizini

Ipo kaskazini mwa wilaya, yenye mwinuko wa kutoka usawa wa bahari wa meta 1,500 – 1,750 (ASL). Nyanda za juu zina udongo wa mfinyanzi wenye rangi nyekundu iliyokolea uliokauka vizuri hadi udongo tifutifu wa kahawia nyekundu ambao una rutuba kidogo. Mvua ni milimita 1000 – 1600 kwa mwaka na inatawanyika vizuri wakati wa msimu wa kunyesha. Kanda ina watu wengi. Mazao yanapandwa kwa wingi ni mahindi, maharage, kahawa na mihogo.

### 1.7.5 Nyanda za juu za Kusini

Ni eneo lenye vilima vyenye miinuko mikali vyenye vijito vinavyokatisha katikati vinavyomwaga maji kwenye Ziwa Tanganyika. Mwinuko unaanzia meta 1500 – 2462 kutoka usawa wa bahari. Kilimo katika kanda hii ni kidogo sana kwa kuwa kuna makazi

machache ya watu kwa mfano kuna kijiji kimoja tu chenye takribani familia 200 zinazojishughulisha na kilimo. Hata hivyo, kanda hii inazalisha sana kahawa.

Kwa ujumla, mvua huanza mwishoni mwa Oktoba na kumalizika Mei na kipindi cha ukame cha karibu majuma mawili mwezi Januari. Kwa ujumla kuna mvua ya mara kwa mara na ya kutosha katika wilaya hii. Upandaji wa mazao ya biashara na ya chakula hufanyika kwa pamoja mwezi Oktoba na Novemba. Aidha, mwezi Februari mazao ya muda mfupi ( kama vile maharage, alizeti, aina fupi za mahindi na viazi) huweza kupandwa.

### 1.8 Hali ya Ardhi

Hali ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inafaa kwa kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara kama vile ndizi, mahindi, mpunga, mihogo, maharage, viazi vitamu, karanga, kahawa, alizeti, matunda na mboga.

Ardhi imegawanywa katika aina nne za udongo ambazo ni mchanga, mfinyanzi, tifutifu yenye rutuba, mchanganyiko wa tifutifu na mfinyanzi. Kutokana na ulimaji wa mara kwa mara katika baadhi ya maeneo, udongo hauna rutuba. Ili kukabiliana na tatizo la udongo kukosa rutuba, wakulima hutumia mboji pamoja na mbolea za viwandani.

### 1.9 Sura ya Nchi

Ardhi inayofaa kulimwa inakadiriwa kuwa zaidi ya kilometa za mraba 10,150 wakati ni asilimia 18 tu ndiyo imendelezwa. Jumla ya eneo linalolimwa linakadiriwa kuwa Km za mraba 1900 na hifadhi za taifa za Mahale na Gombe ni kilometa za mraba 6,613.354, mashamba ya misitu ni hekta 240.9 na hifadhi za misitu asilia ni hekta 494,835.4.

### 1.10 Shughuli za Kiuchumi

Uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma unategemea kilimo zaidi, ambapo ardhi inayolimwa inakadiriwa kuwa Kilometa za Mraba 1,900 $Km^2$ (18.72%) ya jumla ya ardhi yote inayofaa kulimwa. Zaidi ya asilimia 90 ya watu wa Wilaya hii wanategemea zaidi shughuli za kilimo. Hata hivyo, mchango wa sekta ya kilimo kwa Uchumi wa Wilaya umeathiriwa na hali ya hewa isiyotabirika, ikizingatiwa kwamba sekta ya kilimo inategemea mvua. Shughuli nyingine za kiuchumi kama vile ufugaji, uvuvi na utumiaji wa maliasili kama vile misitu na ufugaji wa nyuki hukamilisha shughuli za kilimo za wakazi wa wilaya ya Kigoma.

# SURA YA PILI

## UCHANGANUZI WA HALI HALISI

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea uchanganuzi wa kina wa hali ya zamani na ya sasa ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Aidha, inaelezea uwezo, udhaifu, fursa na vitisho vinavyoikabili Halmashauri. Udhaifu unachukuliwa kama maeneo ya uboreshaji ambayo idara na vitengo mbalimbali vimeweka mikakati yao vya kukabiliana na udhaifu huo. Bado, fursa zinachukuliwa kama maeneo ambayo Halmashauri inaweza kupata faida zaidi na Idara zimeweka malengo na mikakati mbalimbali ya kutumia fursa hizo.

### 2.1 Upitiaji tena wa Utoaji Huduma za uchumi wa Jamii

Kama ilivyo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inakabiliwa na matatizo ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na sababu kadhaa zikiwa ni pamoja na Teknolojia duni, kutokuwa na mtaji, miundombinu duni ya uchumi, Upungufu wa taasisi za elimu ya juu, uhamaji kutoka vijijini kwenda mijini, ongezeko la haraka la idadi ya watu, raslimali chache na mifumo duni ya masoko.

Kwa hiyo, sehemu hii inalenga kupitia kwa ufupi hali ya utoaji huduma za kijamii na kiuchumi kama sehemu ya uchanganuzi wa hali. Upitiaji tena ni wa muhimu sana kwa kuwa unatambua matatizo yaliyopo ya kijamii na kiuchumi na kuiwezesha idara, vitengo mahsusi kuweka malengo na mikakati ya kuyatatua.

#### 2.1.1 Utoaji wa Huduma za Kijamii

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inatoa huduma nyingi za kijamii kwa wadau wake ikiwa ni pamoja na jamii kwa ujumla, jumuiya ya wafanya biashara, Taasisi za Fedha, Wadau wa maendeleo, AZISE, Mashirika ya Kidini, Vyama vya Ushirika, Wakulima, Mawakala, Watoa huduma, Serikali Kuu na wengine. Upitiaji tena wa huduma hizi na hali ilivyo kwa sasa umeonyeshwa kulingana na kila huduma kama ifuatavyo:

#### 2.1.1.1 Elimu

Huduma ya elimu inayotolewa na Halmashauri imegawanywa katika sehemu mbili; sehemu ya elimu ya msingi na sekondari. Hali ilivyo ya huduma ya elimu kulingana na kila sehemu inaonyeshwa kama ifuatavyo:

**A) Elimu ya Msingi**

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, kila kijiji kina shule ya msingi, pamoja na kwamba baadhi ya Vijiji tayari vimejenga shule za msingi zaidi ya moja. Kuna jumla ya shule za msingi 220 (moja ni ya binafsi) wilayani katika mwaka 2012. Hata hivyo, wilaya ina jumla ya wanafunzi 110,175 (52,950 ni wavulana na 57,225 wasichana) na jumla ya madarasa 1,377). Uwiano wa wanafunzi kwa chumba ni 1:80 ikilinganishwa na uwiano unaotakiwa wa 1: 40 katika ngazi ya kitaifa. Kutokana na ukweli huo, kuna upungufu wa madarasa 1,377 katika wilaya. Zaidi ya hayo, kuna madawati 23,126 ambayo ni uwiano wa dawati moja kwa wanafunzi 1:5 badala ya uwiano uliopendekezwa kitaifa wa 1:2.

Vyoo vya mashimo ni 1,560 ambayo ni uwiano wa 1:70. Tatizo la wanafunzi kuacha shule bado ni kubwa sana katika wilaya, ambapo wanafunzi 1,848 (wavulana 949 na wasichana 899) waliacha shule mwaka 2012 ambapo ni asilimia 1.7. Sababu kubwa ni utoro, kupata mimba mapema na mtizamo hasi kuhusu elimu.

Kuna watu 70,267 (Wanawake 39,365 Wanaume 30,962) ambao hawajui kusoma na kuandika. Wilaya ina jumla ya watu 198,255 (wanaume 70,112 na wanawake 128,143) ambao wanahudhuria madarasa ya Watu wazima (2012). Hata hivyo, Wilaya inatarajia kuandikisha watu 567,429 ifikapo 2017.

Kuna walimu 2,025 kwa maana kwamba, daraja la IIIA ni 1,890, na wenye Diploma/Shahada ni 81 na IIIB/C ni 54. Uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi kwa sasa hivi ni 1:54.

Kuna mabadiliko makubwa katika upatikanaji wa vifaa vya kufundishia kama vile vitabu vya kiada, ambapo uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi bado ni mdogo sana kwa mazingira ya kujifunzia, uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu kimoja katika wilaya ni 1:6 kwa mwaka 2012. Shabaha ya Halmashauri ni ongezeko la vitabu angalau kufikia uwiano wa 1:3 ifikapo mwaka 2017.

### B) Elimu ya Sekondari

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ina jumla ya shule za sekondari 39 ambapo shule za serikali ni 32 na shule za binafsi ni 7. Kuna jumla ya madarasa 319 (Shule za serikali) na jumla ya wanafunzi 11,485 (wavulana 6280 na wasichana 520). Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ni 1:36 ukilinganishwa na uwiano wa 1:40 katika ngazi ya kitaifa. Kuna meza za wanafunzi 12,985 na viti 12,985 ambavyo ni uwiano wa meza moja kwa mwanafunzi 1:1 ambapo ni sawa na ngazi ya kitaifa.

Kuna wanafunzi 219 kwa kila choo cha shimo, ambapo ni uwiano wa 1:52; mahitaji ya jumla ya choo cha shimo ni mashimo 623, hivyo kuna upungufu wa vyoo vya mashimo 404 shuleni. Kuna wanafunzi 5,525 walioandikishwa mwaka 2013 kujiunga na kidato cha kwanza ambao miongoni mwao 3,508 ni wavulana na 2,017 ni wasichana.

Kuna walimu 283 (wanaume 261 na wanawake 22) na viwango vyao vya elimu ni diploma – 257 na shahada – 26. Uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi kwa sasa hivi ni 1:40. Uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ni 1:4. Wanafunzi wanaoacha shule bado ni tatizo, sababu kubwa zikiwa ni utoro, mimba, kuolewa mapema, shughuli za uvuvi na mtazamo hasi kuhusu elimu.

### 2.1.1.2 Afya

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma haina Hospitali ya Wilaya, Vipo Vituo vya Afya 6 (vinavyomilikiwa na Serikali) na Zahanati 72 (Zinazomilikiwa na Serikali ni 67). Vijiji vyote isipokuwa 3 vina Zahanati kama Sera ya Afya inavyotaka, lakini Kata 19 hazina vituo vya afya kama inavyotakiwa. Hata hivyo, Kituo cha Afya kipya kinajengwa katika Kata ya Ilagala.

Mahitaji ya jumla ya watumishi wa afya ni 559; hivi sasa kuna watumishi 252 tu (45%) na kwa hiyo kuna upungufu wa watumishi wa afya 307. Halmashauri ina Daktari 1 kama inavyotakiwa na wanachama wa CHMT 7. Daktari wa Meno anakosekana miongoni mwa wanachama wa CHMT. Upungufu mkubwa wa wafanyakazi upo katika kada zifuatazo; waganga wasaidizi 112 kati ya 126, Wauguzi 113, Madaktari wa meno 5, Wasaidizi wa Maabara 2 na Wafamasia wasaidizi 5.

Magonjwa makuu kumi katika Wilaya ni; ARI, Malaria, Nimonia, Kuhara, matatizo ya ngozi matatizo ya macho, mataizo ya kinywa, matatizo ya moyo, PID na matatizo ya shingo ya uzazi. Watoto ndiyo kundi linaloathiriwa sana na magonjwa haya. Upungufu wa wafanyakazi, dawa, vifaa vya tiba na mazingira bora ya huduma za afya ni miongoni mwa matatizo makubwa ya Sekta ya Afya katika Halmashauri. Uboreshaji wa huduma za afya na usambazaji wa dawa ulio sawa katika Huduma za Afya ndiyo kipaumbele cha Halmashauri katika kipindi cha mpango mkakati.

#### 2.1.1.3 Maji

Hivi sasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, asilimia 53.9 ya watu wanapata maji safi na salama ya kunywa kutoka vyanzo mbalimbali vya maji vilivyoboreshwa kama vile; chemchemi, visima vya kina kirefu, mifereji, mito, visima vya kina kifupi na Ziwa. Wilaya inashirikiana na wabia wengine wa maendeleo katika juhudi za kutoa maji safi na salama ya kunywa. Kuna wafanyakazi 17 wenye sifa badala ya 28 wanaohitajika.

### 2.1.2 Utoaji wa huduma za kiuchumi

#### 2.1.2.1 Kilimo

Kilimo ni shughuli kuu ya kiuchumi ya watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Ardhi inayolimwa sasa hivi ni Hekta 182,813.4 au asilimia 18 ya ardhi yote inayolimika ambayo ni Hekari 1,015,630. Takriban kaya 84,274 wanajishirikisha kikamilifu na kilimo ambao ni asilimia 82 ya watu wote wanaolima mazao ya biashara hasa kahawa katika nyanda za juu na mpunga katika nyanda za chini.

Utaratibu mkubwa wa kilimo katika Wilaya ya Kigoma unazingatia ukulima wa kahawa-mahindi-maharage katika nyanda za juu, mahindi-tumbaku katika nyanda za chini na muhogo-mpunga katika ukanda wa Ziwa. Kilimo ndiyo chanzo kikuu cha mapato kwa sababu kinachangia hadi asilimia 91 ya mapato ya Wilaya. Mazao ya biashara ni pamoja na kahawa, tumbaku na michikichi, wakati mahindi, muhogo, maharage, ndizi, mpunga ni mazao ya chakula. Kahawa ni chanzo kikuu katika nyanda za juu na katika eneo la miteremko ya milima wakati mahindi na tumbaku ni vyanzo vikuu vya mapato katika maeneo ya nyanda za chini. Katika pwani ya Ziwa Tanganyika, uvuvi ni chanzo kikuu cha

mapato, hususan katika Tarafa ya Buhingu, na sehemu ya Tarafa za Ilagala, Mwandiga na Kalinzi wakati uvuvi ni chanzo kikuu cha mapato wakati muhogo ni zao la chakula katika eneo hilo. Mazao makuu ya biashara ni; Kahawa, Tumbaku, Mpunga na michikichi, wakati mazao makuu ya chakula ni; Mahindi, Maharage, Muhogo na Mpunga.

Hali halisi ya maofisa ugani wanafikia 46 ambao ni wataalamu katika Nyanja mbalimbali dhidi ya mahitaji ya maofisa uga 86. Kwa hiyo kuna upungufu wa maofisa ugani 40 katika sekta ya Kilimo ambao unasababisha kutokutosheleza kwa huduma za ugani kwa ajili ya wakulima.

#### 2.1.2.2 Mifugo

Wilaya ina mifugo mbalimbali ambayo inajumuisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe. Kwa mujibu wa data za Wilaya za 2010, mifugo iliyopo katika Wilaya ya Kigoma ni Nguruwe (5,631), Ng'ombe (32,390), Mbuzi (248,119), Kondoo (18,852) na Kuku (279,358). Hata hivyo kuwepo kwa mifugo mbalimbali mpaka sasa hakukidhi mahitaji ya bidhaa zake kiasi kwamba mahitaji yake ya ndani yanatoshelezwa na bidhaa za kuingizwa kutoka katika mikoa jirani ya Shinyanga, Tabora na Rukwa ingawa wilaya imejaliwa kuwa na maeneo ya uchungaji ya kutosha.

Hali halisi ya maofisa ugani wa mifugo wanafikia wataalamu 26 katika nyanja mbalimbali dhidi ya mahitaji ya wafanyakazi 81. Kwa hiyo, kuna upungufu wa maofisa ugani katika sekta ya mifugo ambao husababisha kutokutosheleza kwa huduma za ugani kwa wafugaji. Kwa hivi sasa huduma za ugani zinazopatikana wilayani zinajumuisha Majosho 20 ya kuogeshea ng'ombe, vituo 14 vya uendelezaji mifugo na Machinjio 256.

AZISE nyingi zinazofanya kazi katika Wilaya hii kwa sehemu zinatoa mchango mkubwa kwa sekta ya Kilimo, mifugo na sekta nyingine zinazohusiana. AZISE hizo zinajumuisha JGI, FELISA, CARITAS, TCRS, MIBOS, FAO, SODESO, KIVIDEA, KIPAFADA, Uvunaji endelevu na CHAMA CHA USHIRIKA NA MUUNGANO. Kuna masoko mawili (2) ya mifugo na bidhaa za mifugo wilayani kutokana na kuwepo kwa mawasiliano mazuri na pia ukaribu wa wilaya na mpaka wa pamoja na Burundi na Kongo.

#### 2.1.2.3 Vyama vya Ushirika

Wilaya ina jumla ya Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa 80 ambavyo vina wanachama 9,116. Vyama vilivyo hai ni 54 wakati 26 haviko hai, vyama hivyo vinahudumiwa na wafanyakazi 4 badala ya 11 wanaohitajika hivyo kusababisha kutokutosheleza kwa huduma za ushirika.

Vyama vya Ushirika vilivyotajwa hapo juu vimegawanywa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Vyama vya masoko ya Kilimo....................... | 25 |
| (ii) | Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa....................................................................... | 51 |
| (iii) | Ushirika wa Ufugaji wa Nyuki.................................. | 2 |
| (iv) | Biashara ya pamoja................................................................ | 1 |
| (v) | Vyama vya Ushirika wa Mifugo................................ | 2 |
| (vi) | Chama cha Ushirika wa Tumbaku cha Kigoma........... | 1 |

#### 2.1.2.4 Ujenzi

Idara ina wafanyakazi 6 wakati mahitaji halisi ni wafanyakazi 10. Upungufu huu wa wafanyakazi wenye ujuzi umesababisha kuwa na huduma za barabara zisizotosheleza. Wilaya ina Magari 26 (magari makubwa 2 na madogo 24) ingawa ni magari 15 tu ndiyo yanayofanya kazi. Aidha, kuna boti 4 ambazo miongoni mwa hizo 1 ni boti iendayo kasi na pikipiki 117.

Jumla ya mtandao wa barabara Wilayani ni km 832.2, ambazo barabara za Wilaya km 32.2, km 302 ni njia zinazoingia katika barabara kuu. Km. 73 ni za lami, km 222 za kokoto na km 202 barabara za udongo, aina zote mbili ziko chini ya TANROAD. Karibu asilimia 75 ya barabara ziko katika hali nzuri wakati asilimia 20 ziko katika hali ya wastani na asilimia 5 ziko katika hali mbaya. Asilimia 95 ni barabara zinazopitika kwa mwaka mzima wakati asilimia 2.5 hazipitiki wakati wa msimu wa mvua. Zaidi ya hayo, Wilaya haina vifaa vya barabara kama vile Greda na Buldoza kwa ajili ya ukarabati.

#### **2.1.2.5** Maendeleo ya jamii

Kuna wafanyakazi 19 kati ya 36 wanaohitajika wakati ambapo wafanyakazi 8 wanafanya kazi katika ngazi ya Kata. Upungufu wa wafanyakazi umesababisha kuwepo na huduma za Maendeleo ya Jamii zisizotosheleza katika Jumuiya za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma

Wilaya ilianzisha Vikundi 143 vya Kiuchumi katika Jamii, kati ya hivyo 61 ni vikundi vya wanawake na 17 ni vikundi vya vijana na vikundi vingine 65.
Vikundi vilivyopokea mikopo ni 52 na idadi ya wafadhiliwa ni 143 (Wanawake na vijana). Licha ya kupokea mkopo vikundi vyote vimepewa mafunzo kuhusu upangaji na usimamiaji wa mradi ili kuhakikisha kuwa miradi ni endelevu, kipato kuongezeka na hatimaye kiwango cha umaskini kupunguzwa.

#### 2.1.2.6 Maliasili

Wilaya imejaliwa kuwa na Hifadhi za Misitu za Taifa za kutosha kama vile Lugufu ( Hekta 5,439), Ilunde (Hekta 5,997.50), Basanza (Hekta 12,850), Mkuti Magharibi na Mashariki (Hekta 35,612), Uvinza (Hekta 16,835), Mpanda Line ( Hekta 35,612) na Nkungwe Bay (Hekta 5,957). Misitu yote hii iko chini ya Mamlaka ya Serikali. Aidha, kuna hifadhi kubwa ya msitu ambayo iko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya inayofahamika kama hifadhi ya msitu ya Rukunda – Kachambi (Hekta 11,991.70). Wilaya ya Kigoma imefunikwa na uwanda mkubwa wa ukanda wa mbuga, msitu wa Mlima, msitu wa kiikweta unaoambaa kando kando ya mto hususan kandokando ya mto Malagarasi, Ugalla na Msitu wa Masito.

Licha ya hifadhi hizi za misitu, Wilaya ya Kigoma ina eneo kubwa la Wazi (Eneo la Wazi la Uvinza), eneo la ardhi oevu (Eneo la Malagarasi – Moyovosi Ramsar) na eneo la hifadhi la Wanyama pori (Eneo la hifadhi la Wanyama pori la Luganjo) lililopo katika Taarafa za Uvinza na Nguruka; Pia kuna maziwa makubwa kama vile Ziwa Tanganyika ( kilometa za mraba 8,029), Ziwa Sagara na Nyamagoma katika Taarafa za Nguruka; na Mito ya kudumu kama Mto Malagarasi, Ugalla na Lugufu. Ni wilaya hii ndiyo ina tishio kubwa la wanyama mwitu kama vile Sokwe, Tembo na Wadudu wengine na Ndege.

Wilaya ina Hifadhi za Taifa mbili zinazoitwa Gombe na Mahale ambazo ziko chini ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa za Tanzania na hifadhi moja ya Wanyama pori inayodhibitiwa inayoitwa Luganzo. Aidha, Wilaya inapakana na hifadhi ya Wanyama pori ya Moyovosi Kigosi chini ya Mkurugenzi wa Wanyama pori katika eneo la Kaskazini. Hili ni eneo la kuendeleza vivutio kwa watalii na shughuli za utalii/uwindaji.

Katika programu ya upandaji misitu, miti 226,454 ilipandwa katika mwaka 2011/2012 na jumuiya (JKT, Shule za Msingi na Sekondari, AZISE, Asasi za Kiraia za Jamii, Asasi na sekta binafsi).

Idara ya Maliasili ina sekta nne ambazo ni Uvuvi, Misitu, Wanyama pori na Ufugaji nyuki pamoja na wafanyakazi 26 badala ya 46 hivyo kusababisha usimamiaji wa Maliasili usiotosheleza.

#### 2.1.2.7Ardhi

Sekta hii inapaswa kuwa na wafanyakazi 32 wenye sifa, lakini ina wafanyakazi 12 tu kiasi kwamba inakuwa vigumu kuhudumia wilaya nzima. Idara imepanga kuongeza idadi ya Hati Miliki kuanzia 117 katika mwaka 2012/13 hadi 1500 katika mwaka 2016/17 na kuongeza ukusanyaji mapato kuanzia 26,000,000 katika mwaka 2012/13 hadi 58,000,000 ifikapo 2016/17.

Idara imepanga kuongeza idadi ya viwanja vilivyopimwa kuanzia 12301 katika mwaka 2012/13 hadi 17,000 ifikapo 2016/17. Aidha, kuna mpango wa kuongeza idadi ya mipaka ya vijiji iliyopimwa kuanzia 75 hadi 78 ifikapo 2016/17. Idara pia imepanga kuongeza idadi ya mashamba yaliyopimwa kuanzia Hekta 12,500 katika mwaka 2012/13 hadi Hekta 18,500 ifikapo 2016/17. Hata hivyo, kuongezeka kwa michoro ya mipango miji kuanzia 7 katika mwaka 2012/13 hadi 27 ifikapo 2016/17 litakuwa ni jambo la kupewa kipaumbele. Idara imepanga kuongeza idadi ya vijiji vyenye mpango wa kutumia ardhi kuanzia 60 katika mwaka 2012/13 hadi 78 ifikapo 2016/17 na kuongeza idadi ya hati za hakimiliki kuanzia 1165 katika mwaka 2012/13 hadi 6165 ifikapo 2016/17.

#### 2.1.2.8 Utawala na Utumishi

##### A) Utawala

Wilaya ina idara 12 na vitengo 6 vyenye zana na vifaa vya kufanyia kazi. Wafanyakazi waliopo katika utawala ni 3,038 badala ya 4,322 wanaohitajika. Upungufu huu umesababaisha:-

- Kuwa na wafanyakazi wachache wenye sifa zinazotakiwa.
- Mgawanyo wa majukumu kwa wafanyakazi ambao hawajapatiwa mafunzo ya majukumu hayo.
- Kiwango kidogo cha utoaji huduma katika baadhi ya sekta.
- Ofisi na samani zisizotosha katika ngazi zote.
- Mfumo wa Usimamiaji Habari usiofaa (MIS)

### 2.1.2.9 Mipango

Shughuli yake kuu ni kuratibu mipango yote ya wilaya, kukusanya data za kiuchumi na kijamii na kuzichambua kwa niaba ya idara mbalimbali za Halmashauri. Aidha, kuratibu ujumuishaji wa ripoti, kuzisambaza kwa wadau husika, kusimamia, kufuatilia na kutathmini miradi ya maendeleo. Hivi sasa idara ina wafanyakazi 6 ambao wanatosha kutekeleza ipasavyo majukumu ya idara.

### 2.1.2.10 Fedha na Biashara

Idara ya fedha na biashara inatekeleza kazi zake kwa kufuata Mkataba wa Fedha wa 1997 na majukumu makuu yanayofanywa yakiwa ni pamoja na:-

- Kuishauri Halmashauri kuhusu masuala ya fedha
- Kubuni vyanzo vipya vya mapato
- Kukusanya mapato yote ya wilaya
- Kuhakikisha kuna matumizi mazuri ya mapato
- Kufanya majumuisho ya ripoti za fedha
- Kutunza orodha zote za raslimali za kudumu za halmashauri

Idara ina wafanyakazi 15 wakati mahitaji halisi ni wafanyakazi 21 hali ambayo inasababisha kukosa ufanisi katika huduma za fedha.

### 2.1.2.11Ukaguzi wa Hesabu wa Ndani

Hali kadhalika kama ilivyo katika idara ya biashara na fedha, sehemu ya ukaguzi wa hesabu wa ndani inatekeleza kazi zake kwa kufuata Mkataba wa fedha wa 1997. Majukumu makuu ya sehemu ya Ukaguzi wa Hesabu wa Ndani ni pamoja na haya yafuatayo:-

- Kuishauri halmashauri kuhusu masuala yote ya fedha
- Kufanya ukaguzi wa hesabu wa ndani wa hesabu za wilaya na kusimamia na kutoa ushauri ipasavyo.

Kuna wafanyakazi 3 kati ya 6 wanaohitajika ambapo matokeo yake ni kukosa ufanisi katika huduma za ukaguzi wa hesabu.

### 2.1.2.12 Masuala ya Kisheria

Kudumisha na kuwezesha amani, utulivu na utawala bora, ambavyo vinaendeleza Ustawi wa Jamii na kustawi kwa uchumi wa watu wote katika eneo lake la kisheria sambamba na sheria,

sera na kanuni za kitaifa. Halmashauri ina mwanasheria 1 mwenye sifa badala ya 2 wanaohitajika kutekeleza masuala ya kisheria.

#### 2.1.2.13 Kitengo cha Kusimamia Ununuzi

Kinatekeleza kazi zake kwa kufuata Sheria ya Ununuzi wa Umma (PPA) ya 2004 na Kanuni ya Ununuzi wa Umma ((PPA) ya 2005, na majukumu makuu ni Kusimamia shughuli za Ununuzi (PMU). Kitengo cha Kusimamia Ununuzi kina wafanyakazi 5 lakini mahitaji halisi ni wafanyakazi 6. Upungufu wa mfanyakazi mmoja siyo tatizo kubwa sana la kuweza kuathiri kazi za idara.

#### 2.1.2.14 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ina sehemu ya TEHAMA iliyo hai yenye wafanyakazi wataalamu wawili. Inafanya kazi katika idara zote katika kutatua matatizo mbalimbali ya TEHAMA. Hata hivyo kitengo hiki hakina muundo na mpangilio mzuri kiutawala na mkuu wa sehemu hahusishwi kabisa katika CMT, Mikutano ya Fedha na mikutano yote ya halmashauri. Aidha, kitengo hakina sera zenye mfumo mzuri, sheria na kanuni za kuiongoza sehemu ya TEHAMA

Pamoja na matatizo yote haya, sehemu hii iko mbioni kuanzisha Tovuti ya Wilaya, Blogi, kutengeneza na kutekeleza programu za kompyuta, mwunganisho wa mtandao Ofisini na upatikanaji wa Intaneti Wilayani. TEHAMA ina lengo la kuwawezesha wafanyakazi katika sehemu hii kupata mafunzo kadhaa ili kukabiliana na mabadiliko ya TEHAMA na kuendeleza teknolojia mpya duniani.

#### 2.1.2.15 Masuala Mtambuko

Yapo baadhi ya mambo ambayo lazima yaingizwe kwenye mkondo mkuu wa programu za jumla za maendeleo za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma; vinginevyo maendeleo yake ya baadaye yanaweza kuwa hatarini. Hivyo kuna umuhimu wa kuingiza kwenye mkondo mkubwa, na hili linajumuisha masuala ya tabianchi, jinsia, ugonjwa wa VVU/UKIMWI na magonjwa mengine yanayozuka kama vile kisukari, shinikizo la damu na ugonjwa unaotokana na maji. Pia kumekuwepo na ongezeko la yatima ambalo ni tatizo kubwa linalohitaji kushughulikiwa.

## MASUALA MENGINE MUHIMU

### (a) Umaskini

Takriban asilimia 90 ya watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma wanaishi vijijini na wanategemea kilimo kwa maisha yao. Shughuli kuu za kiuchumi zinazofanyika katika wilaya hii ni pamoja na kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara ndogondogo, viwanda vidogovidogo, ajira rasmi na zisizo rasmi. Kilimo ni cha kujikimu kutokana na utumiaji wa zana duni; aidha, uvuvi bado ni wa kizamani. Kuna kiwango cha ukuaji unaoendelea wa umaskini miongoni mwa watu walio wengi ambao wanategemea shughuli za kilimo kutokana na mabadiliko ya tabianchi, utumiaji wa teknolojia, pembejeo za kilimo na masoko.

### (b) VVU/UKIMWI

Vipengele vingi vimechangia katika kuongezeka kwa matukio ya maambukizo mapya ya VVU. Mwaka 2012, watu waliopimwa VVU/UKIMWI walikuwa 8,773 (3,804 walikuwa Wanaume na 5,853 walikuwa Wanawake) ambao miongoni mwao 83 (Wanaume 23 na Wanawake 60) walikuwa na maambukizo ambapo ni 0.01%. Watu walioambukizwa ambao wanatumia ARV ni 504 ( 181 ni Wanaume na 323 ni Wanawake). Hususan katika baadhi ya maeneo kama vile Nguruka, Uvinza, Ilagala na Kasuku kuna ongezeko la maambukizo mapya hasa miongoni mwa wanawake na wanaume walio katika umri wa kuzaa kati ya 18 na 45. Sababu kubwa ni umaskini miongoni mwa jamii, ngono isiyo salama, ulevi wa pombe na dawa za kulevya na maingiliano kwa sababu za kibiashara.

### (c) Jinsia

Idadi kubwa ya watu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni Wanawake. Kwa mujibu wa sensa ya 2002, wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya jumla ya idadi yote ya watu. Halmashauri inapanga kuhamasisha vikundi vya kiuchumi vya wanawake na kuwasaidia mikopo midogomidogo kutoka katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto. Mikopo hii inatolewa kupitia Programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake inayotekelezwa chini ya Wizara hii.

Hata hivyo, kuna changamoto muhimu ambazo zinajumuisha; fedha zisizotosha kuhusiana na mahitaji na idadi inayoongezeka ya wanawake, kushindwa kwa baadhi ya wanawake kurejesha mkopo uliotolewa ili wengine waweze kupewa mikopo na ujuzi mdogo wa kiujasiriamali kulingana na muundo wa masoko.

## 2.2 Raslimali kuu zilizopo

Wilaya ya Kigoma imejaliwa kuwa na maliasili nyingi ambazo zinajumuisha; Misitu ya Taifa, Mbuga za Wanyama za Taifa, Hifadhi za ardhi oevu na hifadhi ya Wanyama pori. Raslimali nyingine muhimu ni Ziwa Tanganyika, Nyamagoma, Sagara na mito mikubwa kama vile; Malagarasi, Luguvu na Ugalla. Hata hivyo Wilaya ina fahari ya kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba, mifugo na madini hasa katika chumvi.

### 2.2.1 Ardhi

Ardhi ni raslimali na ni muhimu sana kama nguzo kuu ya uchumi wa Wilaya. Hata hivyo, hivi sasa, eneo linalotumika kwa kilimo ni Hekta 182,813.4 ambalo ni asilimia 18 ya ardhi yote inayofaa kwa kilimo. Wawekezaji wakuu wa kilimo ni Agrisol (Hekta 13,600), WAMA (Hekta 516), FELISA (Hekta 4,200) na wengine ambao waliwekeza katika ukubwa wa kati (Hekta 80) kila moja.

### 2.2.2 Misitu:

Wilaya ya Kigoma imejaliwa kuwa na Misitu mingi ya Taifa kama vile; Lugufu (Hekta 5,439), Ilunde ( Hekta 5,997.50), Basanza (Hekta 12,850), Uvinza (Hekta 16,835), Mpanda Line (Hekta 35,439), Nkungwe Bay (Hekta 5,957), Mkuti Mashariki na Magharibi, Rukunda – Kachambi (Hekta 11,991.70).

### 2.2.3 Wanyama pori:

Wilaya ya Kigoma ni mojawapo ya wilaya zenye bioanuwai Kubwa nchini Tanzania. Ina utajiri wa wanyama pori hususan Tembo, Kulungu, Mamba, Mbelele, Kiboko, Samba, Chui, Nyani, Nyati, shoe bill na Korongo. Ni moja ya wilaya zenye idadi kubwa ya wanyama pori hatari kama vile Sokwe, yangeyange, na Korongo. Wilaya ina Mbuga za wanyama za Taifa mbili (Mahale na Gombe), Hifadhi za Misitu saba (Lugufu, Ilunde, Basanza, Uvinza, Nkungwe Bay na Mpanda Line ambazo zina eneo la Hekta 118,303.50. Hifadhi moja ya Wanyama (Moyowosi – Kigosi), hifadhi mbili za wanyama pori zinazodhibitiwa (Mfubasi na Luganzo). Maeneo mengine muhimu ni eneo Ardhi oevu (Malagarasi – Moyoyosi Ramsra). Uchungaji wa kupindukia, Uchomaji mkaa, Ukataji magogo ya mbao, uvuvi haramu, na ujangili ni tishio kubwa kwa maendeleo endelevu ya bioanuwai.

### 2.2.4 Ufugaji nyuki

Ufugaji nyuki unafanywa kwa kiwango kidogo vijijini na sasa hivi unashika kasi kutokana na mafunzo yanayotolewa kwa wanavijiji na viongozi wa vijiji kuhusu umuhimu wa ufugaji wa nyuki katika uchumi. Katika kulinganisha, uzalishaji wa asali na nta umeongezeka kuanzia tani 48.9 na tani 3.2 hadi tani 102.4 na tani 7.2 katika mwaka 2008 na 2009. Bado uzalishaji unahitaji kuongezwa kwani mahitaji ya nje ni makubwa zaidi kuliko uzalishaji.

Kuna watu 1,630 (Wanaume 1070 na Wanawake 560) Wanaojihusisha na ufugaji wa nyuki. Aidha, kuna jumla ya mizinga ya kisasa 3,450 na ya kizamani 9,350 katika wilaya. Sekta ya ufugaji nyuki haijafanikiwa vya kutosha kiasi cha kuchangia katika kipato cha jamii kuinua uchumi wa wilaya kwa ujumla. Ili kuboresha sekta hii, halmashauri ya wilaya inalenga kuongeza idadi ya wafuga nyuki hadi 2,500 na mizinga ya kisasa 10,000 ifikapo mwaka 2017.

### 2.2.5 Uvuvi

Tasnia ya uvuvi ina dhima muhimu katika uchumi wa Wilaya. Shughuli za uvuvi hufanywa zaidi katika Ziwa Tanganyika ambalo lina eneo la kilometa za mraba 8,029, mabwawa madogo ya maji ya Ziwa Sagara na Nyamagoma, Mito Malagarasi, Ugalla, na mabwawa ya Luguvu na Kandaga.

Kuna takriban wavuvi 8,096 wanaofanya shughuli ya uvuvi wakati wote na wanaofanya kwa muda kwa kutumia mitumbwi 4,095 iliyojengwa kulingana na utafiti wa Mfumo wa Uvuvi wa 2011. Idadi ya samaki waliovuliwa katika mwaka 2008 ilikuwa tani 66,195, ambao waliingiza kiasi cha jumla ya shilingi za Kitanzania 64,722,337,301//=, hiki ni kiwango cha chini cha idadi kubwa iliyovuliwa ya tani 65,000. Spishi zilizovuliwa kwa wingi ni Dagaa na Migebuka.

Aidha, Wilaya ya Kigoma ni maarufu kwa uzalishaji wa samaki wa kuweka kwenye matangi kwa ajili ya kuuzwa Ulaya na mahali pengine kwenye masoko ya dunia. Huzalisha karibu tani 10 kwa mwaka. Kuna Makampuni 2 tu yanayojaribu uvuvi wa aina hii.

Wilaya ni maarufu katika ufugaji wa samaki katika nyanda za juu za kaskazini kwa kiwango cha chini. Hii ni kutokana na imani kwamba ufugaji wa samaki hauwezi kuwa wa kibiashara.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya bado anawaelimisha na kuwahamasisha watu kufanya hivyo, kwa kuwa ni mbadala wa protini ya samaki katika maeneo ya mbali.

Ufugaji wa majini ni mbadala wa uvuvi uliopindukia katika Ziwa, na hivyo, unahitaji kutekelezwa kikamilifu. Hata hivyo, uvuvi katika Ziwa Tanganyika uko chini kwani ni asilimia 50 tu inayotekelezwa kwa mwaka. Vifaa vya kisasa na vinavyofaa katika mazingira vinapaswa kutumiwa kulingana na vifaa vya usindikaji samaki.

### 2.2.6 Utalii:

Tasnia ya utalii inaendelezwa kwa kiwango kidogo sana katika Wilaya ya Kigoma pamoja na kuwepo kwa vivutio kadhaa kama vile; Sokwe na spishi za pekee za ndege katika mbuga za wanyama za Taifa za Mahale na Gombe, fukwe za Ziwa za mchanga na za wazi. Mji wa Kigoma una hoteli nyingi za kitalii za gharama nafuu, malazi na chakula kizuri. Baadhi ya hoteli hizi ni; Lake Tanganyika, Hill top, Coast View na Mwaka hill. Kwa kushirikiana na Serikali kuu na wadau wengine tayari Wilaya imeanza kuboresha miundombinu ambayo itavutia watalii zaidi katika siku zijazo.

Kuna Hoteli tatu za viwango vya juu zilizojengwa katika mbuga za wanyama za Taifa za Mahale katika maeneo yanayovutia sana. Hizi ni pamoja na; Fly Catcher view Lodge, Sinsidar Lodge na Kangwena safari Lodge kwenye Ufuko wa Ziwa Tanganyika katika sehemu ya Kaskazini ya Wilaya ya Kigoma. Zipo pia Hoteli mbili za viwango vya juu zilizojengwa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Gombe ambazo ni; Hill top tented Camp, na Gombe Hotel, zote mbili zikiwa kwenye Ufuko wa Ziwa Tanganyika katika sehemu ya Kaskazini ya Wilaya ya Kigoma.

Hoteli zote hizi ni za gharama nafuu, malazi mazuri na chakula kizuri. Kihistoria, Kigoma ni mwisho wa safari ya Dkt. Livingstone alipokuwa akisafiri kutoka Bagamoyo (Mkoa wa Pwani), hivyo, tasnia ya utalii inahitaji kuendelezwa na kukuzwa katika Wilaya ya Kigoma na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla.

Kuhusu utalii ambao unahusiana na kutazama wanyama, kuna maeneo mengi wilayani kama vile; mbuga za wanyama za Taifa za Mahale na Gombe, Hifadhi za Wanyama pori za Moyowosi – Kigosi, Hifadhi kubwa ya misitu, Maeneo ya hifadhi ya wanyama pori ya Luganzo na Mfubasi. Vivutio vingine ni; Ziwa Tanganyika ambalo ni la pili duniani kwa kina kirefu, kumbukumbu ya Dkt. Livingstone, Mv. Liemba ambayo ni meli ya zamani sana ya

Wajerumani (zaidi ya miaka 100 ambayo bado inafanya kazi), Eneo la ardhi oevu la Ramsar, Chemchemi ya asili ya maji chumvi kandokando ya mto Luchugi katika Tarafa ya Uvinza, na maporomoko ya maji ya Igamba Miembeni katika mto Malagarasi.

### 2.2.7 Madini

Wilaya ina utajiri mkubwa wa raslimali za madini, ambapo baadhi bado hayajachimbwa. Madini maarufu yanayopatikana katika Wilaya hii ni pamoja na; Chumvi. Inachimbwa katika Kata ya Uvinza, karibu Kilomita 110 kutoka Mji wa Kigoma. Uzalishaji wa wastani kwa mwaka ni karibu tani 20,650.

Platinamu na Nikeli, Gallen na Shaba katika Kata ya Ilagala, Chokaa katika vijiji vya Kazuramimba na Uvinza hupatikana kwa wingi katika kijiji cha Mgambazi, Gallen na shaba katika Kata ya Ilagala, Chokaa katika vijiji vya Kazuramimba na Uvinza, na Dhahabu katika Kata za Kalya na Buhungu. Migodi hii bado haijachimbwa kwa kiasi kikubwa.

### 2.3 Uchanganuzi wa Wadau

Uchanganuzi na matarajio ya wadau umeelezwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

### Jedwali 2.3.1 Uchanganuzi wa Wadau

***(Tini: Upangaji wa Vipaumbele; J =Juu , K =Kati na C =Chini )***

| JINA LA MDAU | MATARAJIO | ATHARI KAMA MATARAJIO HAYAJAFIKIWA | UPANGAJI KWA VIPAUMBELE (J,K&C) |
|---|---|---|---|
| **JAMII** | • Kuboresha viwango vya maisha ya jamii pamoja na utoaji huduma za kiuchumi za jamii kwa wakati na kwa ufanisi. | -Kuendelea kwa umaskini.<br>-Utoaji wa huduma zisizotosheleza. | J |
| **JUMUIYA YA WAKULIMA NA WAFANYA BIASHARA** | • Kuongezeka kwa mazao ya kilimo na mapato na matumizi kibiashara.<br>• Kuboresha usafiri na mtandao wa mawasiliano. | -Uzalishaji duni wa kilimo.<br>-Hasara kiuchumi kutokana na kushindwa kupata masoko. | J |
| **SERIKALI KUU (MOF, PMO-RALG, POPEE) NA RAS** | • Kutekeleza mkakati wa kupunguza umaskini, Kilimo, ufugaji, na sera za ushirika, kufuata miongozo ya ASDP.<br>• Utumiaji wa soko la pamoja la JAM, kufikia kuwa na upatikanaji wa kutosha wa chakula.<br>• Utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.<br>• Uthabiti mkubwa wa uchumi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. | - Wananchi kuwa na picha mbaya kwa serikali, kiwango cha juu cha mfumko wa bei. | C |
| **WATUMISHI WA UMMA** | • Mazingira bora ya kazi. | Utendaji mbovu katika utoaji huduma. | K |
| **AZISE NA WADAU WA MAENDELEO.** | • Kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika kutoa huduma kwa jamii (PPP). | Utendaji mbovu katika kutoa huduma. | K |
| **WANASIASA** | • Kuboresha utoaji wa huduma za jamii na | Kupoteza Imani ya | C |

| JINA LA MDAU | MATARAJIO | ATHARI KAMA MATARAJIO HAYAJAFIKIWA | UPANGAJI KWA VIPAUMBELE (J,K&C) |
|---|---|---|---|
| | kiuchumi kwa jamii.<br>• Utawala bora<br>• Utekelezaji wa ilani ya uchaguzi | Wapiga kura<br>Kuongezeka kwa mgogoro wa kiitikadi | |
| **VYOMBO VYA HABARI** | Habari nyingi nzuri za kutolewa taarifa | Sura mbaya ya halmashauri | C |
| **TAASISI ZA KIELIMU** | • Uandikishaji zaidi wa wanafunzi kutokana na kuongezeka kwa uwezo wa kulipa ada | Uandikishaji mdogo | C |
| **MDAs** | • Kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutekeleza sera za nchi | Utoaji wa huduma mbaya kwa jamii | J |
| **VYAMA VYA USHIRIKA** | • Kuongezeka kwa umuhimu wa huduma za mikopo midogomidogo na masoko | Vyama visivyo hai | K |
| **BUNGE** | • Utawala bora, amani na utulivu na utawala wa sheria | Kuyumba | J |
| **KUNDI LILILO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU** | • Kuboresha huduma maalum pamoja na fursa kwa ajili yao | Utoaji wa huduma mbaya na kukosa fursa | J |
| **WAFUGAJI** | • Kuongeza idadi na ubora wa mifugo na bidha za mifugo | Kuendeleza umaskini | J |
| **TAASISI ZA FEDHA** | • Kuboresha shughuli za ukopeshaji | Kuongezeka kwa umaskini | C |

### 2.4 Uchanganuzi wa SAOC

**UWEZO, MAENEO YA KUBORESHA, FURSA NA CHANGAMOTO**

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| **RASLIMALI WATU NA UTAWALA** | • Timi yenye sifa<br>• Ari ya kazi katika timu<br>• Kushirikiana majukumu na sehemu nyingine<br>• Mfumo madhubuti wa uongozi unaoshuka hadi chini katika ngazi ya vijiji na vitongoji.<br>• Kuwepo kwa sheria ndogondogo zilizoanzishwa katika ngazi za wilaya na vijiji. | • Kutokutoshelaza kwa ofisi katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya VEOs & WEOs<br>• Vifaa vichache vya kazi<br>• Wafanyakazi kutokuwa na ufanisi katika kutumia vifaa vipya vya kazi<br>• Nyumba chache za wafanyakazi katika maeneo ya vijijini<br>• Mawasiliano baina ya idara yasiyotosheleza | • Kupatikana kwa wabia wakuu wa maendeleo, wahisani na taasisi za fedha<br>• Kupatikana kwa fursa za uwekezaji<br>• Ujenzi wa miundombinu uliopendekezwa na unaoendelea kv. Barabara ya Kigoma – Dodoma, Kiwanja cha ndege nk.<br>• Aina za mali asili kv. Mbuga za wanyama za taifa, hifadhi za wanyama pori | • Kuongezeka kwa kiwango cha uhamisho wa watumishi<br>• Matatizo na wafadhili katika kutafuta fedha<br>• Msingi mbovu wa kiuchumi katika jamii<br>• Mifumo ya mawasiliano na usafiri isiyotoshelez a kimkoa |
| **MIPANGO YA UCHUMI & TAKWIMU** | • Uongozi wa Idara una uzoefu mkubwa katika baadhi ya halmashauri<br>• Idara ina mchanganyiko wa jinsia na taaluma mbalimbali kulingana na kazi za Idara<br>• Idara ni imara katika kuratibu | • Uandikaji usiotosheleza wa ripoti za M&E, uandikaji wa mpango wa biashara, mawasiliano ya kimkakati na ujuzi wa kushawishi<br>• Mfumo usiotosheleza wa M&E<br>• Kutokuwa na | • Kuanzisha Kamisheni ya ya Taifa ya Mipango<br>• Kuimarisha uratibu baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu, RALG,Rs, HAZINA na NPC<br>• Kuwepo na Programu ya Misaada ya | • Kuwa na ratiba isiyo na uhakika ya kuwezesha mipango na utekelezaji na utoaji taarifa<br>• Kushuka kwa Uchumi Duniani<br>• Halmashauri kutegemea kwa kiasi kikubwa |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | shughuli kubwa za kitaifa na kieneo<br>• Mgao mkubwa wa madaraka na ufanyaji kazi wa pamoja miongoni mwa wanaidara<br>• Timu ina wepesi wa kushirikiana na idara nyingine mara inaposhirikishwa<br>• | mawasiliano ya kutosha na Timu ya Wasaidizi<br>• Vyanzo vya data visivyo na uhakika katika kutekeleza kazi za Idara<br>• Maeneo ya ofisi yamechakaa na hayatoshi na hivyo kusababisha msongamano wa wafanyakazi katika ofisi | mabadiliko ya Milenia.<br>• Kuwepo kwa miongozo ya mipango ya Kitaifa<br>• Kuwepo kwa huduma za ushauri katika maeneo mapya ya shughuli za Serikali<br>• Kuwepo kwa watu wa Kigoma katika Uongozi wa juu wa PMO RALG, HAZINA na NPC<br>• Utashi chanya wa Rais na Waziri Mkuu katika kuisaidia Kigoma<br>• Upatikanaji wa wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza Kigoma kv. Madini, Benki, Agric, NSSF, TIB, Machimbo ya nk. | bajeti ya Serikali Kuu/Wahisani/ na AZISE<br>• Takwimu za idadi ya watu zisizo na uhakika kwa ajili ya mipango kutokana na kumiminika kwa wahamiaji |
| **KILIMO, UMWAGILIAJI NA VYAMA** | • Usimamizi wa idara za juu una ushurikiano | • Timu ina mpango mkakati na utekelezaji wa | • Upatikanaji wa Mkakati na sera ya Kilimo | • Majanga ya asili |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| **VYA USHIRIKA** | mkubwa, mgawanyo wa kazi na kufanya kazi kwa pamoja<br>• Malalamiko machache sana kutoka kwa maofisa Kilimo wa Kata na Vijiji kwenda Makao Makuu/DED<br>• Idadi kubwa ya SACCOs, Vyama vya Ushirika na Ubia.<br>• Kuwa na watoa huduma za ugani 76 wa ndani<br>• Kuwepo kwa vituo zaidi ya 4 vya kutolea maarifa ya kilimo<br>• Upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuanzisha mipango ya umwagiliaji<br>• Timu ina urahisi wa kushirikiana na idara nyingine na kuchukua majukumu ya nyongeza | ujuzi wa miradi usiotosheleza.<br>• Uratibu wa wadau wa sekta ya ndani hautoshi kv. Sehemu za Ushirika, Ardhi, na Biashara<br>• Mpaka usioeleweka kati ya idara na idara mpya ya Mifugo na Uvuvi<br>• Wakulima hawalimi kilimo cha kibiashara<br>• Mfumo wa M&E usiotosheleza katika maeneo makuu ya matokeo ya sekta<br>• Mashine chache kwa ajili ya kuwezesha kilimo cha kisasa<br>• Miundo na ujuzi usiotosha kuhakikisha kuna utoshelevu wa chakula kipato kwa ajili wananchi kwa mwaka mzima | Kwanza<br>• Utayari wa Suma JKT na makampuni mengine ya vifaa kufanya kazi Kigoma<br>• Upatikanaji wa mvua za kutosha na za kuaminika<br>• Upatikanaji wa Miradi ya Kitaifa kv. DASIP, DADIP nk.<br>• Upatikanaji wa nguvu kazi ya kutosha kuendesha shughuli za kilimo<br>• Uhaba wa ardhi nchini Burundi na muda na utayari wa Kongo wa kushiriki katika kilimo<br>• Upatikanaji wa huduma za mikopo za Taifa<br>• Upatikanaji ya wa ardhi ya kutosha yenye rutuba isiyotumika | • Uhamaji wa mifugo kutoka kwenye maeneo ya ukame<br>• Maendeleo ya haraka na ufunguaji wa masoko bila ya mkakati wa utayari<br>• Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa bado hazijauelewa mfumo wa benki ya ardhi kwa ajili ya utekelezaji<br>• Mifumo mibovu ya zana za Kilimo inayofaa hali ya hewa ya Kigoma<br>• Uchumi hafifu wa wakulima<br>• Milipuko wa magonjwa ya mazao na wadudu wa mifugo |
| **MIFUGO NA** | • Uongozi wa Juu | • Upangaji wa | • Upatikanaji wa | • Uhamaji wa |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| **UVUVI** | una wahitimu wote kwa sekta zote mbili na wanawajibika katika kazi zao<br>• Sekta zote mbili zina maofisa kilimo na asasi (BMU za kutosha na Umoja wa Wafugaji)<br>• Kuwepo kwa watoa huduma za ugani 76 katika eneo<br>• Timu ina urahisi wa kushirikiana na idara nyingine na kuchukua majukumu ya nyongeza | kimkakati na ujuzi wa miradi ya utekelezaji visivyotosha<br>• Uratibu usiotosha wa wadau wakuu wa ndani wa sekta hususan katika LLGAs<br>• Mipaka isiyo dhahiri katika kazi kati ya idara na idara mpya ya Kilimo DNROLU<br>• Data na miundombinu isiyoaminika kwa ajili ya kusaidia sekta zote mbili<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo ya matokeo muhimu ya sekta<br>• Idadi isiyodhibitika ya mifugo | masoko nchini Burundi, Kongo na Zambia<br>• Ardhi ya kutosha kwa ajili ya mifugo na ziwa, mito na mabwawa kwa ajili ya uvuvi<br>• Upatikanaji wa Miradi ya Kitaifa ya DASIP, DADIP nk<br>Upatikanaji wa huduma za mikopo za Taifa<br>• Ushirikiano wa kitaasisi na SIDO na VETA katika shughuli za maendeleo<br>• Kuwepo kwa spishi tofauti za samaki hivyo kupanua soko | mifugo<br>• Maendeleo ya haraka na kufungua masoko bila ya mkakati wa utayari<br>• Kuwepo kwa maharamia katika Ziwa Tanganyika.<br>• Hasara kubwa baada ya mavuno katika bidhaa za uvuvi kutokana na teknolojia duni<br>• Hatari ya mabadiliko ya tabia nchi<br>• Majanga asilia<br>• Migogoro baina ya wafugaji &watumiaji wengine wa ardhi |
| **ARDHI MALIASILI NA MAZINGIRA** | • Kuwepo kwa maofisa wenye uzoefu na HoD wapya wenye uzoefu<br>• Timu inaweza kubadilika na wakati wote inaomba kufanya kazi na idara | • Hakuna gari la kuwezesha kwenda sehemu mbalimbali<br>• Upungufu wa vifaa vya ugani mfano mahema<br>• Mipaka isiyo wazi katika shughuli kati ya idara na | • Maeneo ya kutosha yasiyokaliwa yenye ramani na yasiyo na ramani<br>• Kuwepo kwa asasi ya ardhi Tabora karibu na mkoa wetu<br>• Kuwepo kwa | • Majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu<br>• Utoaji mdogo wa wataalamu nchini<br>• Uhamaji wa mifugo na watu |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | nyingine<br>• Mipango muhimu na vifaa vya upimaji vinapatikana pamoja na kompyuta za kutosha<br>• Ushirikiano imara kati ya Wafanyakazi mwega na HoD wao<br>• Asasi za misitu zenye utaratibu katika kijiji<br>• Kuwepo kwa maofisa wapya wa utalii wenye sifa na ujuzi ili kuendeleza utalii wakiongeza thamani katika sekta ndogo zote | idara mpya ya Mifogo na uvuvi, kitengo cha Ufugaji nyuki na mazingira<br>• Maofisa wanasambazwa na hakuna ofisi ya umiliki wa usajili wa ardhi ya halmashauri.<br>• Mifumo isiyofaa ya Ufuatiliaji & Tathimini katika maeneo ya matokeo muhimu ya sekta<br>• Usimamiaji duni wa ardhi katika ngazi ya kijiji katika maeneo yaliyopangwa<br>• Usimamizi duni katika fuko za ziwa<br>• Wafanyakazi wachache katika menejimenti ya ardhi, wanyamapori na misitu<br>• Utaratibu mbaya wa ufuatiliaji wa kodi ya ardhi ya Halmashauri | AZISE iliyo tayari kufanya kazi na Halmashauri katika sekta ndogo zote<br>• Masoko makubwa ya ndani na ya kimataifa ya bidhaa ndogo<br>• Ushirikiano na uratibu wa NEMC<br>• Huduma za mikopo ya taifa kupatikana ili kugharimia kueneleza sekta ndogo zote | • Mfumo wa hifadhi ya ardhi bado haujaeleweka na Serikali Kuu pamoja na katika Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji |
| **UJENZI** | • Timu ina uzoefu wa kutosha wa ugani kwa maeneo yote<br>• Timu ina vifaa vya | • Kuna gari moja tu kwa ajili ya shughuli za ugani na za kiofisi<br>• Mipaka isiyo wazi | • Huduma za mikopo za taifa zinapatikana kugharimia na kuendeleza sekta | • Kutotosheleza kwa msaada wa Rs katika kusimamia kazi za idara |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | kutosha vya kufanyia kazi<br>• Mafundi wa ndani wasiotosheleza ambao wanaweza kupata mafunzo<br>• Utayari wa Timu kwa ajili ya mabadiliko na maboresho<br>• Idara zina nafasi ya kutosha kwa ajili ya shughuli za nje na za ofisini<br>• Timu ina ujuzi wa kompyuta | katika shughuli kati ya idara na Idara ya Jumuiya na PMU<br>• Usimamizi wa mkataba usiotosheleza<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo ya matokeo muhimu ya sekta<br>• Kutojihusisha ipasavyo kwa jamii kabla na wakati wa utekelezaji<br>• Utunzaji mbaya wa kumbukumbu na mawasiliano na Idara nyingine, hasa PMU na Mipango | • Kuwepo kwa vifaa na njia mbadala za ujenzi mfano matofali<br>• Kuwepo kwa njia mbadala za usafiri mfano, njia ya reli, ya majini na anga<br>• TANROAD kuwa tayari kushirikiana na halmashauri, mfano kushirikiana rasilimali watu, taarifa, huduma za maabara n.k.<br>• Kupatikana kwa fedha kutoka mfuko wa barabara na vyanzo vingine | • Utoaji mdogo wa wataalamu nchini<br>• Msaada duni wa taasisi za Serikali kuu kama TAMESA,TTCL,TANESCO<br>• Majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu |
| **PMU** | • Timu ina uzoefu wa kutosha wa ugani katika maeneo yote<br>• Timu imechanganya jenda<br>• Walio wengi katika Timu wanafahamu kompyuta<br>• Mazingira ya kazi ni mazuri | • Wajumbe wa Timu walio wengi wanapaswa kuripoti katika Idara zao za sekta, HoD na HPMU<br>• Zana na vifaa vya kufanyia kazi havitoshi<br>• HPMU anakaimu na bado hajateuliwa<br>• Mawasiliano duni kati ya | • Kuwepo kwa miongozo na hatua za wazi<br>• Kuwepo kwa huduma za mtandaoni<br>• Kuwwepo kwa asasi za udhibiti kama vile GPSA<br>• Kuwepo kwa njia tofauti za usafiri, wa reli, majini, barabarana anga ili kuwezesha | • Kushuka kwa kuaminiwa kwa watoa huduma kutokana na deni kubwa<br>• Kwa sasa kuna ushindani mdogo miongoni mwa watoa huduma, na makandarasi<br>• Utoaji mdogo wa wataalamu |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | | wafanyakazi wa PMU na idara nyingine<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo ya matokeo muhimu ya sekta<br>• Wajumbe wa timu hawana majukumu ya kazi | usafirishaji wa vifaa vilivyonunuliwa<br>• Msaada wa PPRAS katika kudhibiti taratibu, michakato na viwango | katika nchi<br>• Ukosefu wa elimu ya ununuzi kwa watoa huduma |
| **BIASHARA NA FEDHA** | • Vyanzo kadhaa muhimu vya fedha kubainishwa<br>• Kuwepo kwa mfumo wa EPICOR kusaidia malipo<br>• Wajumbe wa Timu walio wengi wanafahamu kompyuta<br>• Timu imechanganya jinsia kwa uwiano<br>• Umahiri mzuri katika utunzaji hesabu<br>• Uongozi wa juu una uzoefu wa kutosha | • Vifaa na zana za kufanyia kazi havitoshi<br>• Wajumbe wa timu hawana ujuzi wa aina nyingi<br>• Utunzaji kumbukumbu na mawasiliano duni na wadau wa ndani na nje<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo ya matokeo muhimu ya sekta<br>• Mtandao wa intaneti usio imara kuweza kusaidia mifumo ya EPICOR na Lawson<br>• Mifumo duni na miundombinu michache kuwezesha ukusanyaji wa kodi | • Kuwepo kwa msaada kutoka HAZINA,NBBA na CAG katika kudhibiti taratibu za fedha<br>• Kuwepo kwa miongozo na hatua za wazi<br>• Uzalishaji mkubwa wa nguvu kazi kwa kada ya kati na ya chini<br>• LACC na Ukaguzi mwingine wa kudhibiti zinadhibiti mfumo<br>• Huduma za mikopo za Taifa kuwepo ili kugharimia na kuendeleza sekta za Uchumi<br>• Kuwepo kwa huduma za | • Utoaji mdogo wa wataalamu wa kiwango cha juu katika nchi<br>• Viwango vya maadili vilivyoshuka katika ngazi ya chini ya mamlaka ya serikali<br>• Ukosefu wa elimu ya biashara kwa wafanyabiashara<br>• Imani za kishirikina katika shughuli za biashara<br>• Ukaidi wa jumuiya ya wafanyabiashara kulipa ushuru wa soko |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | | • Idadi na ubora usiotosheleza wa wafanyakazi katika sekta ya biashara<br>• Umahiri usiotosheleza katika usimamizi wa fedha na uwekezaji pamoja na katika kuendeleza biashara na uwekezaji | mtandao na Rs kwa ajili ya kusaidia shughuli za EPICOR | |
| **MAENDELEO YA WATU NA USTAWI WA JAMII** | • Wajumbe wa timu wanaweza kuendana na mabadiliko na mazingira ya kufanyia kazi na jamii<br>• Nafasi ya kutosha ya ofisi kwa ajili ya kufanyia kazi<br>• Wajumbe wa timu walio wengi wanafahamu kompyuta<br>• Timu ina mchanganyiko wa jinsia wenye uwiano<br>• Menejimenti ya juu ina uzoefu wa kutosha katika utaalamu na maeneo ya kufanyia kazi | • Kutojituma vya kutosha kwa wafanyakazi katika ngazi ya chini ya Serikali<br>• Ujuzi wa maandalizi ya mradi usiotosheleza<br>• Vifaa na zana za kazi zisizotosheleza<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo muhimu ya utekelezaji wa matokeo<br>• Utunzaji kumbukumbu na mawasiliano duni na wadau wa ndani na nje | • Kuwepo kwa miongozo ya wazi, hatua na sera<br>• Kuwepo kwa vikundi vya vijana na wanawake<br>• Programu za taifa za TACAID na TASSAF kuzisaidia Idara<br>• Kuwepo kwa AZISE zilizo tayari kushirikiana na idara<br>• Kuwepo kwa udongo unaofaa na ardhi inayotumika kwa ajili ya vikundi vya kilimo | • Wahisani wa kimataifa wasioratibiwa kuwasiliana moja kwa moja na jamii<br>• Ushawishi wa kisiasa<br>• Majanga ya asili mfano mafuriko, ukame n.k.<br>• Kuchelewesh wa kwa fedha kutoka serikalini kwa ajili ya shughuli za idara |
| **ELIMU – SEHEMU YA** | • Kuanzishwa kwa | • Mazingira duni ya | • Programu ya | • Mchango duni |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| **MSINGI NA SEKONDARI** | sekta ya elimu isiyo rasmi ili kuendeleza elimu ya sekondari<br>• Vijiji vilivyo vingi vina michezo (Timu ya mpira wa miguu na kikundi cha utamaduni)<br>• Ushirikiano imara na timu ya kazi baina ya Idara za Elimu ya sekondari<br>• Idara ina vifaa vya ofisi vya kutosha<br>• Menejimenti ya juu ina uzoefu wa kutosha katika utaalamu na maeneo ya kufanyia kazi<br>• Kamati/Bodi za shule zinazofanya kazi kikamilifu<br>• Kuwepo na kutolewa kwa ruzuku maalumu kwa kila mtu<br>• Kuwepo kwa umeme wa jua katika shule za sekondari zilizo nyingi<br>• Kuwepo kwa Maabara zinazohamishika | kufanyia kazi na ya kuishi kwa wafanyakazi katika ngazi ya chini<br>• Ujuzi wa ufundishaji usiotosheleza kwa wafanyakazi wa ngazi ya chini<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo muhimu ya matokeo ya utekelezaji<br>• Vifaa vya kufundishia na kujifunzia visivyotosheleza<br>• Uhaba wa walimu katika ngazi zote mbili, msingi na sekondari<br>• Mfumo duni wa mawasiliano | Taifa ya LCDG na TASAF kusaidia idara mbalimbali<br>• Uwezekano wa kupata wafanyakazi wa nyongeza kupitia programu za kubadilishana za kimataifa<br>• Kuwepo kwa wanazuoni wa Kigoma wanaotaka kujitolea kutoa huduma zao<br>• Kuwepo kwa vyuo vya walimu na Vituo vya Kupatia Maarifa vya Walimu | wa wenyeji katika maendeleo ya elimu<br>• Mtazamo hasi wa jamii katika elimu<br>• Imani za uchawi<br>• Malalamiko na masharti ya vyama vya wafanyakazi na vikundi rika<br>• VVU/UKIMWI ambao unaathiri nguvu kazi za idara |
| **MAZINGIRA, AFYA NA USAFI** | • Sekta ni miongoni mwa maeneo ya vipaumbele | • Hakuna ofisi iliyobainishwa kwa ajili ya Idara | • Mafanikio ya Rwanda katika eneo la usafi | • Majanga ya asili na yanayosababis |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | vikubwa vya Halmshauri hivyo kutoa uzingativu maalumu<br>• Huduma za usafi zina bajeti mahususi katika idara ya afya<br>• Idara ina mchanganyiko wa jinsia wenye uwiano | • Hakuna uongozi wa Idara (HoU)<br>• Vifaa na zana za kufanyia kazi zisizotosheleza<br>• Mfumo wa M&E usio na ufanisi katika maeneo muhimu ya matokeo ya utekelezaji<br>• Ujuzi usiotosheleza katika kutekeleza shughuli za urejelezaji na uchambuzi | yanatoa jukwaa kwa idara kujifunza mbinu zao<br>• Kuwepo kwa AZISE zilizo tayari kushirikiana na idara<br>• Uwezekano wa Idara kuchangisha fedha kutoka vyanzo vya afya na mazingira<br>• Kuwepo kwa miongozo na Hatua na sera zilizo wazi | hwa na binadamu<br>• Ukosefu wa vyuo vya ufundi vya kutosha<br>• Ukosefu wa viwanda kwa ajili ya kurejeleza bidhaa za plastiki<br>• Ufahamu mdogo wa jamii ya wenyeji kuhusu masuala ya mazingira na usafi |
| **AFYA** | • Ufuataji wa kiwango cha juu katika kutekeleza programu za afya kulingana na miongozo<br>• Kuwepo kwa idadi ndogo ya wafanyakazi wenye sifa na waliopata mafunzo<br>• Vituo vya afya kuwepo katika kila kijiji<br>• CHMT kufanya kazi katika timu yenye ari nzuri | • Fursa za mafunzo na ufundishaji tena zisizotosheleza<br>• Ushirikiano duni kutoka katika sehemu/idara zinazosaidia hivyo kuathiri utendaji wa programu za afya<br>• Ugharimiaji mdogo katika programu za afya<br>• Idadi kubwa ya wafanyakazi wasio na mafunzo katika ngazi ya uendeshaji | • Upangaji wa watumishi kutoka serikali kuu<br>• Kuwepo kwa sera na miongozo katika programu za sekta ya afya<br>• Kuwepo kwa wabia wa kufanya nao kazi (AZISE)<br>• Unyeti wa sekta katika programu za Serikali hivyo kupewa kipaumbele<br>• Kuratibu viongozi kama MSD | • Usafirishaji wa magonjwa kutoka nchi za jirani<br>• Ushawishi wa kisiasa<br>• Majanga ya asili<br>• Kutoa kwa wakati usiofaa fedha kutoka Serikalini ili kutekeleza miradi ya afya |
| **UKAGUZI WA** | • Wafanyakazi | • Bajeti ndogo | • Mwongozo na | • Ukosefu wa |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| **NDANI** | wenye sifa na mahiri katika idara<br>• Kazi nzuri ya pamoja na ushirikiano miongoni mwa wanaidara<br>• Taratibu za ndani zinazofaa kufanya kazi<br>• Kuwepo kwa msaada na ushirikiano ndani ya idara | katika kuwezesha kazi za kitengo kwenye ngazi za kijiji<br>• Vifaa na huduma za kazi visivyotosheleza<br>• Ukosefu wa majengo ya ofisi<br>• Baadhi ya vijiji kuwa ndani sana na ugumu wa kuvifikia | Hatua ya wazi kusimamia shughuli za Idara<br>• Kuwepo kwa mamlaka za usimamizi kama vile wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa serikali (GAG), NBAA n.k.<br>• Kuwepo kwa asasi za mafunzo nchi nzima ili kutoa wataalamu mahiri | uaminifu miongoni mwa wanajamii<br>• Kiwango kikubwa cha udanganyifu na ukosefu wa maadili katika jamii<br>• Utoaji wa wakati usiofaa wa fedha zilizotengwa kutoka serikali kuu |
| **SHERIA** | • Mtaalamu wa Sheria mwenye ujuzi<br>• Ushirikishanaji mzuri wa majukumu na sehemu nyingine<br>• Mfumo imara wa kisheria na kiutawala ili kusimamia shughuli mbalimbali.<br>• Kuwepo kwa sheria ndogondogo zilizoanzishwa na kanuni nyingine katika ngazi ya wilaya na kijiji. | • Vifaa vya kufanyia kazi visivyotosheleza<br>• Kiwango kidogo cha wafanyakazi<br>• Fursa chache za mafunzo ya kujiendeleza na kozi fupi kuongeza ujuzi wa sheria | • Kuwepo kwa sheria za nchi na sera, miongozo na kanuni za sekta<br>• Kuwepo kwa asasi nyingine ili kusaidia utawala bora na utawala wa sheria kama vile Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (PCCB), Jeshi la polisi n.k.<br>• Idadi ya asasi za mafunzo kutoa wafanyakazi wa sheria wenye ujuzi | • Kushuka kwa mtazamo wa maadili na kuenea kwa vitendo vya udanganyifu katika jamii<br>• Ukosefu wa elimu na taratibu za sheria kwa wanajamii walio wengi<br>• Mabadiliko ya uwanja wa sheria kuhusiana na sheria na kanuni. |
| **TEHAMA** | Kuwepo kwa wafanyakazi wataalamu wa TEHEMA. | Ongezeko la idadi ya wafanyakazi<br>Uandaaji wa tovuti ya halmashauri ya | Wachuuzi wa miundombinu ya TEHAMA<br>TTCL | Wataalamu wa kompyuta.<br>Kutofaa kwa mfumo wa M&E katika maeneo |

| IDARA/SEHEMU | UWEZO | MAENEO YA KUBORESHA | FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| | | Wilaya<br><br>Ufungaji mitandao ya mawasiliano baina ya idara.<br><br>Msaada wa mfumo, huduma na mafunzo ya mtumiaji wa mwisho. | Mshauri mwelekezi wa TEHAMA. | muhimu ya utekelezaji wa matokeo.<br><br>Hakuna mkuu wa sehemu<br><br>Kujihusisha kusikofaa katika utoaji uamuzi ngazi ya juu kuhusiana na sehemu ya TEHAMA |
| **UCHAGUZI** | • Uzoefu mkubwa katika Serikali za Mitaa, na Uchaguzi Mkuu<br>• Ushirikishanaji mzuri wa majukumu na sehemu nyingine<br>• Kuwepo kwa sheria za uchaguzi, miongozo na kanuni. | • Watumishi wasio na sifa<br>• Ukosefu wa ofisi kuu na ofisi za kufanyia kazi zisizotosheleza maeneo ya vijijini kwa VEOs & WEOs<br>• Vifaa vya kufanyia kazi visivyotosheleza<br>• Wafanyakazi wapya kutomudu kutumia zana za kufanyia kazi<br>• Gharama pungufu wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa | • Kuwepo kwa wabia wakuu wa maendeleo, wahisani na asasi za fedha<br>• Miundombinu iliyopendekezwa na inayoendelea kujengwa mfano,barabara ya Kigoma–Dodoma, Uwanja wa ndege n.k. | • Watumishi wachache wenye sifa<br>• Mazingira magumu ya kupata fedha kutoka kwa wafadhili<br>• Ujumuishaji wa siasa wakati wa utaratibu wa uchaguzi<br>• Mifumo ya mawasiliano na usafiri isiyotosheleza kimkoa<br>• Gharama zisizotoshele za wakati wa uchaguzi mkuu |

# SURA YA TATU

# DIRA, DHAMIRA, MALENGO NA MAADILI YA MSINGI

## 3.0 Utangulizi

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni miongoni mwa wilaya za Tanzania ambayo ilianzishwa mwezi Julai1984. Kijiografia, Wilaya iko katika latitudo 4º25 na 6º30 Kusini na kati ya longitudo 29º45 na 31º30 Mashariki. Wilaya imepakana na Burundi upande wa Kaskazini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upande wa Magharibi na Kusini inapakana na Mkoa wa Rukwa.

## 3.1. Dira

Dira ya Halmashauri ni: "inaazimia kuwapatia wakazi wake maendeleo endelevu pamoja na miundombinu iliyoboreka, mawasiliano na upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi ifikapo 2025"

## 3.2 Dhamira

Dhamira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni "kuimarisha uwezo wake yenyewe na ule wa taasisi za kijamii ili kuweza kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi na miundombinu inayofaa kwa kushirikiana na wabia wengine wa maendeleo ndani ya vigezo vya utawala bora".

## 3.3 Maadili ya Msingi

Ili Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ijenge mazingira mazuri na kutimiza Dira na Dhamira yake, maadili ya msingi yafuatayo ni muhimu sana na yataiongoza Halmashauri katika kufikia malengo yake:

- ***Matumizi yanayofaa ya rasilimali zilizopo:*** kuhakikisha rasilimali zinazomilikiwa na Halmashauri zinatumiwa ipasavyo na kwa manufaa kwa kulenga maeneo ya kipaumbele.

- ***Kuongeza ushiriki wa jamii:*** Kuongeza na kuendeleza msaada na ushirikiano wa jamii katika kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

- ***Kazi ya pamoja:*** Kufanya kazi wakati wote katika shughuli mbalimbali kama timu ili kuwa na tija ya hali ya juu kwa kutumia kiasi cha rasilimali cha kutosha.

- ***Utawala bora:*** Kuhakikisha utawala bora katika ngazi zote za utawala kwa kulenga katika ushirikiano wa haki na usawa na wadau wote.

- ***Kujituma kwa kiasi kikubwa katika utoaji huduma*:** kuweka jitihada za kujitolea katika kutoa huduma kwa jumuiya pamoja na msisitizo katika ubora.

- ***Uadilifu:*** Kuwa mfano katika mwenendo wetu na kufanya kazi kwa uaminifu na bila ya upendeleo katika shughuli zetu zote.

- ***Uwazi:*** Kuwa wazi katika kazi na shughuli zetu zote na kuwa tayari kwa uchunguzi wa umma.

### 3.4 Maeneo ya Matokeo muhimu (KRAs)

Haya ni maeneo ya matokeo au maoni muhimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Kwa maneno mengine haya ni maeneo ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inatafuta kupata matokeo kwa manufaa ya jamii nzima. KRA yaliyobainishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma yanajumuisha yafuatayo:

1. Kuongeza vyanzo vyake vya mapato katika halmashauri
2. Huduma nzuri za kijamii na kiuchumi.
3. Ushiriki wa jamii katika kubainisha vipaumbele vyao vya maendeleo katika wilaya.
4. Matumizi yanayofaa ya rasilimali za umma
5. Kuwepo kwa utawala Bora
6. Kuendeleza Amani na Usalama
7. Kuongeza matumizi endelevu ya maliasili na usimamizi wa mazingira
8. Kiwango cha ubora wa huduma kilichoimarishwa

#### 3.4.1 Kuongeza vyanzo vyetu vya mapato katika Halmashauri

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inapata fedha kutoka Serikali Kuu kupitia bajeti ya mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Hata hivyo, fedha kutoka katika chanzo hicho hazitoshi kutoa huduma kwa wanajamii wote matokeo yake Halmashauri imekuwa ikitumia vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuzalisha fedha za ziada ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa wanajamii zaidi. Katika miaka ya hivi karibuni gharama za kutoa huduma na wingi wa huduma zinazotakiwa vimeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na mfumuko wa bei na kuongezeka kwa watu. Kwa hali hiyo, moja ya Maeneo Muhimu ya Matokeo ya Halmashauri ni kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza fedha kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wanajamii.

### 3.4.2 Huduma nzuri za kijamii na kiuchumi:

Hali ya utoaji huduma inaridhisha kwa watu walio wengi katika Wilaya. Katika sekta ya Elimu, uandikishaji wa watoto uko katika asilimia 86. Uwiano wa wanafunzi kwa darasa katika shule ya msingi ni 1:80 ambao uko juu kuliko kiwango cha taifa cha 1:40. Uwiano wa dawati moja kwa wanafunzi ni 1:5 ambao uko juu kuliko kiwango cha taifa. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi kwa sasa ni 1:56; uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi mmoja ni 1:6 badala ya 1:1 kiwango cha taifa.

Wakazi wa halmashauri ya mji wanaopata huduma ya maji ndani ya mita 400 wako 345,276 (53.1%) ya jumla ya idadi ya watu. Katika kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi, Mpango Mkakati wa miaka mitano unadhamiria kuongeza huduma katika sekta za Elimu, Afya, Maji na miundombinu ya Usafiri na nyingine.

### 3.4.3 Ushiriki wa Jamii katika Ubainishaji wa Vipaumbele vya Maendeleo ya Wilaya:

Ushiriki wa jamii katika mipango, usimamizi na utekelezaji wake ni moja ya vigezo katika mipango endelevu na ushiriki. Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikiiwezesha jamii na viongozi wake katika mchakato mzima wa ubainishaji wa vipaumbele vya maendeleo kupitia utoaji wa mafunzo katika mipango shirikishi.

Lengo la halmashauri ya wilaya ni kuanzisha na kuboresha mafunzo hayo kwa viongozi wa ngazi ya kijiji na kata, ili kuimarisha kiwango cha ushiriki wa jamii katika kubainisha vipaumbele vya maendeleo yao kwa uendelevu.

### 3.4.4 Matumizi yanayofaa ya Rasilimali:

Halmashauri ya wilaya ya Kigoma imejaliwa rasilimali mbalimbali kama vile ardhi yenye rutuba kubwa, mifugo, hifadhi ya wanyama pori na vivutio vya utalii, ziwa Tanganyika, madini na rasilimali watu. Halmashauri ya wilaya inadhamiria kuboresha na uongezaji wa jamii kumiliki na kutumia rasilimali zilizopo kwa busara kwa maendeleo endelevu.

### 3.4.5 Utekelezaji wa Utawala Bora:

Halmashauri ya wilaya imekuwa ikitekeleza mihimili ya utawala bora kwa kuimarisha na kuwahusisha wananchi kikamilifu katika ufanyaji uamuzi kupitia mikutano mbalimbali. Lengo la halmashauri ya wilaya ni kuongeza demokrasia, uadilifu, ushiriki, utawala bora na utawala wa sheria.

### 3.4.6 Kuendeleza Amani na Usalama

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imekuwa ikihamasisha amani na usalama ili kuhakikisha jamii inaishi katika uelewano hasa ukichukulia ukweli kwamba wilaya imepakana na nchi zilizokumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe kama Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kwa hali hiyo, uendelezaji wa amani na usalama ni moja ya KRA muhimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

### 3.4.7 Kuongeza matumizi endelevu ya rasilimali na usimamiaji wa mazingira.

Matumizi ya maliasili yanaongezeka kutokana na maendeleo ya teknolojia. Matumizi endelevu ya maliasili, usimamizi wa mazingira na shughuli za usafi vinasisitizwa katika maeneo ambako kuna uchimbaji wa madini. Kama sheria inavyotaka, utekelezaji wa sheria za mazingira unafanyika katika shughuli za maendeleo zinazofanyika katika wilaya ili kuhakikisha athari zinapunguzwa. Jamii ya Kigoma inasisitizwa kufuata taratibu za usafi ili kuwalinda na athari za kiafya.

### 3.4.10 Kuongeza kiwango cha Huduma Bora

Ili kuhakikisha kufaa, ufanisi na uwazi katika utoaji huduma kwa jamii, Uongozi wa Halmashauri ya Kigoma na wafanyakazi wanawajibika katika ari ya kufanya kazi kwa pamoja. Halmashauri imeandaa mkataba wa huduma kwa mteja ambao utaziongoza idara mbalimbali za Halmashauri na vitengo katika utoaji wa huduma.

### 3.5 Malengo ya Pamoja

Katika kipindi cha Mpango Mkakati huu, Halmashauri inajitahidi kufikia malengo yafuatayo:-

A. Kiboresha huduma na kumpunguza maambukizo ya VVU/UKIMWI
B. Kuongeza, kuendeleza na utekelezaji unaofaa wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa
C. Kuboresha upatikanaji, ubora na usawa wa utoaji wa huduma za jamii
D. Kuongeza wingi na ubora wa huduma za jamii na miundombinu
E. Kuendeleza utawala bora na huduma za utawala
F. Kuboresha ustawi wa jamii, jinsia na uwezeshaji wa jamii
G. Kuboresha usimamizi wa dharura na majanga

# SURA YA NNE

# MALENGO MKAKATI, SHABAHA NA MIKAKATI

**4.0 Utangulizi**

Jedwali hili linaeleza uhusiano kati ya Malengo ya Pamoja, Malengo Mkakati, shabaha za utendaji, mikakati, viashirio muhimu vya utendaji, njia za uthibitisho pamoja na ofisa anayehusika kwa kila mkakati uliyotajwa. Ni kutokana na jedwali hili ambapo shughuli zitaandaliwa kwa kuzingatia mikakati kwa kila lengo. Shughuli zitaunda sehemu ya utekelezaji wa mikakati hivyo kuongoza katika uandaaji wa bajeti.

**4.1 IDARA: MIPANGO**

**Lengo la Pamoja**: Kuimarisha upatikanaji wa utoaji wa huduma za jamii zilizo bora na zenye usawa.

| NA. | Malengo Mkakati | Shabaha | Mikakati | Viashirio muhimu vya utendaji | Njia za uthibitisho | Ofisa anayehusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Upatikanaji, Ubora na utoaji wa huduma zenye usawa kuimarishwa kwa asilimia 80 ifikapo Juni 2017 | Kuongeza idadi ya vijiji ambavyo vinaweza kuandaa mipango yao vyenyewe kutoka 45 hadi 78 ifikapo 2017 | - Kuhusisha serikali za vijiji & kata kupitia mikutano ya kushauriana (VEOs, WEOs) kwa kutumia chombo cha O& OD. | Mipango 33 ya vijiji kuandaliwa | -Kuwepo kwa mipango 78<br>-Kuwepo kwa kumbukumbu za vijiji na kata | DPLO |
| | | Kuongeza miradi inayotekelezeka katika wilaya kutoka 150 hadi 750 ifikapo 2017 | -Kuihusisha jamii kupitia kamati ya ujenzi ya kijiji, chini ya usimamizi wa WEOs naVEOs. | -Miradi 500 kuanzishwa | Kuwepo kwa miradi mbalimbali 500<br>Kumbukumbu za serikali za vijiji na WDC<br>-Ripoti za Mradi | DPLO |
| | | Kuongeza idadi ya miradi inayosimamiwa | -VEOs & WEOs kusimamia miradi yote katika maeneo | -Ripoti za maendeleo za | Kuwepo kwa ripoti za robo mwaka | |

| NA. | Malengo Mkakati | Shabaha | Mikakati | Viashirio muhimu vya utendaji | Njia za uthibitisho | Ofisa anayehusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kutoka 150 hadi 750 ifikapo 2017 | yao<br>-Timu ya Ufuatiliaji&Tathimini ya Wilaya | miradi | | DPLO |
| | | Uandaaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka kwa wakati kila mwaka hadi 2017 | -Kuhusisha idara/sehemu nyingine zote na ushiriki wa jamii katika mchakato wa bajeti | -Nyaraka za Bajeti | -Kuwepo kwa waraka wa MTEF<br>-Kumbukumbu za bajeti ya Baraza<br>-DCC, baraza la wafanyakazi na kumbukumbu za RCC | DPLO |
| | | Uandaaji kwa wakati (robo mwaka) wa ripoti za utekelezaji wa mradi ifikapo 2017 | -Kuwahusisha WEOs na Idara/Sehemu nyingine katika uandaaji wa ripoti kwa wakati & uwasilishaji<br>-M&E robo mwaka | Ripoti za utekelezaji wa miradi | -Kuwepo kwa nakala za ripoti<br>-Barua ya kukubali/utambuzi | DPLO |

## 4.2 IDARA: MAENDELEO YA JAMII

**Lengo la Pamoja:** Kuboresha ustawi wa jamii, jinsia na uwezeshaji wa jamii

| NA. | Malengo Mkakati | Shabaha | Mikakati | Viashirio Vikuu vya Utendaji | Njia za Uthibitisho | Ofisa Anayehusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuongeza idadi ya Kamati za Watoto walio katika Mazingira magumu zaidi kutoka 10 mwaka 2012/2013 hadi 78 ifikapo 2016/2017 | Kamati za watoto walio katika mazingira magumu zaidi kuongezeka kutoka 10 hadi 78 ifikapo 2016 /2017 | -Kuendesha mikutano 50 ya kuongeza uelewa na VGs , AZISE na jamii<br>Kuendesha mafunzo ya siku3 kwa VGs 50 AZISE na wanajamii | - Kuanzishwa kwa MVCC 68<br>- Kuendeshwa kwa mafunzo<br>-Kufanyika kwa mkutano | -Idadi ya MVCC kuanzishwa<br>-kumbukumbu za mkutano na karatasi za mahudhurio<br>-Ripoti za mafunzo | SWO |
| 2. | Kuongeza idadi ya vikundi vya kupambana na mila zilizopitwa na wakati kutoka 2 mwaka 2012/2013hadi 20 ifikapo 2016/2017 | Desturi zilizopitwa na wakati kupungua kutoka asilimia 50 hadi 80 ifikapo 2016/2017 | Kuendesha mikutano 20 ya kuongeza uelewa kuhusu mapambano dhidi ya mila zilizopitwa na wakati pamoja na Viongozi wa Dini, VGs & na wanajamii | -Kumbukumbu za mkutano na karatasi za mahudhurio | Kuwepo kwa vikundi vilivyoundwa | SWO |
| 3. | Kuongeza idadi ya vikundi vya uzalishaji vya wanawake na vijana kutoka 120 mwaka 2012/2013 hadi 800 ifikapo 2016/2017 | Vikundi vya Wanawake & Vijana kuongezeka kutoka 120 hadi 800 ifikapo 2017 | Kuwezesha mafunzo ya siku 20 ya kuunda vikundi 20 kwa VGs, Wanawake & Vijana ifikapo 2017 | Ripoti za mafunzo na karatasi za mahudhurio | -Kumbukumbu za mkutano<br>-Karatasi za mahudhurio | DO I |
| 4. | Kuongeza idadi ya miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na jamii kutoka 15 mwaka | Miradi ya maendeleo kuongezeka kutoka 15 mwaka 2012/2013 hadi 40 | Kuwezesha kampeni za kuongeza ufahamu kuhusu uanzishaji wa miradi & menejimenti | Kuwepo kwa miradi iliyoanzishwa | Ripoti za kampeni za uelimishaji | DCDO |

| NA. | Malengo Mkakati | Shabaha | Mikakati | Viashirio Vikuu vya Utendaji | Njia za Uthibitisho | Ofisa Anayehusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2012/13 hadi 40 ifikapo 2016/2017 | ifikapo2016/2017 | pamoja na 200 VGs, AZISE & Wanajamii | | | |
| 5. | Kuongeza AZISE na Asasi za Kiraia ( CBOs) zinazofanya shughuli mbalimbali za uchumi jamii kutoka 70 mwaka 2012/2013 hadi 600 ifikapo 2016/2017 | Idadi ya AZISE & CBOs zinazotoa huduma za uchumi jamii kuongezeka kutoka 70 mwaka 2012/13 hadi 600 ifikapo 2017 | Kuwezesha kampeni za kuongeza uelewa katika uanzishaji wa AZISE/CBOs | Kuwepo kwa idadi ya AZISE/CBOs | Ripoti za kampeni | DCDO |
| 6. | Kuongeza idadi ya kamati za kupambana na maambukizo ya VVU/UKIMWI kutoka 20 mwaka 2012/2013 hadi 104 ifikapo 2016/2017 | Kamati za kupambana na VVU/UKIMWI kuongezeka kutoka 20 mwaka 2012/2013 hadi 104 ifikapo 2016/2017 | Kuwezesha mafunzo ya Kamati za kupambana na VVU/UKIMWI | Ripoti ya uundaji<br>Mafunzo yamefanyika | Idadi ya kamati zilizoundwa<br>Karatasi za mahudhurio | CHAC |
| 7. | Kuongeza idadi ya vikundi vya uzalishaji vya wenye VVU/UKIMWI kutoka 2 mwaka 2005 hadi 10 ifikapo 2011/12 | Vikundi vya uzalishaji vya wenye VVU/UKIMWI kuongezeka kutoka 2 mwaka 2012/ 13 hadi 10 ifikapo 2016/2017 | Kuendesha elimu ya kuongeza uelewa kuhusu uundaji wa vikundi na kuviendeleza<br><br>Kuwezesha mafunzo ya siku 5 ya ujasiriamali kwa vikundi vya uzalishaji vya wenye VVU/UKIMWI | Idadi ya vikundi vya uzalishaji vya wenye VVU/UKIMWI vilivyoanzishwa<br>Karatasi za mahudhurio | Ripoti ya mafunzo<br>-kumbukumbu za mkutano na karatasi za mahudhurio | CHAC |
| 8. | Kuongeza idadi ya wadau (AZISE-CBOs) wanaojihusisha na kampeni za kupambana | Wadau wa Kupambana na VVU/UKIMWI (AZISE, CBOs, | Kuendesha mikutano na wadau ili kubainisha (AZISE, CBOs FBOs | Idadi ya AZISE, CBOs na FBOs kuongezeka | Ripoti ya mkutano<br>Ripoti ya usimamizi na | CHAC |

| NA. | Malengo Mkakati | Shabaha | Mikakati | Viashirio Vikuu vya Utendaji | Njia za Uthibitisho | Ofisa Anayehusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | na VVU/UKIMWI kutoka 31 mwaka 2005 hadi 96 ifikapo 2011/12 | FBOs) kuongezeka kutoka 31 mwaka 2012/13 hadi 96 ifikapo 2016/2017 | zinazojihusisha na kupambana na VVU/UKIMWI<br>Kusimamia na kufanya tathmini katika shughuli zao | | tathmini | |
| 9. | Kuongeza idadi ya vikundi vya shughuli za kiufundivilivyoelimishwa kuhusu Uambukizo kwa njia ya ngono (STIs) kutoka 225 mwaka 2005 hadi 1120 ifikapo 2011/12 | Vikundi vya shughuli za kiufundi vilivyoelimishwa katika STI kuongezeka kutoka 225 mwaka2012/13 hadi 1120 ifikapo 2016/17 | Kuendesha mkutano wa kuongeza ufahamu katika STI pamoja na VG kwa vijiji 75<br>Kuendesha mafunzo kuhusu uundaji na uendelezaji wa kikundi<br>Kuendesha mafunzo kuhusu STI kwa vikundi vilivyoundwa | Vikundi 895 vya shughuli za ufundi vimeelimishwa<br>Mafunzo yameendeshwa<br>Mkutano umefanyika | -kumbukumbu za mkutano na karatasi za mahudhurio<br>Ripoti ya mafunzo | DO II TECH |
| 10. | Kuongeza idadi ya vikundi vinavyotengeneza matofali ya udongo na sementi kutoka 18 mwaka 2005 hadi 90 ifikapo 2011/12 | Vikundi vinavyotengeneza matofali ya sementi na udongo kuongezeka kutoka 18 mwaka 2012/13 hadi 90 ifikapo 2016/2017 | Kuwezesha mkutano wa kuongeza uelewa kwa VG kuhusu matofali ya sementi na udongo kwa vijiji 75<br>Kuendesha mafunzo ya siku 3 kwa vikundi kuhusu utengenezaji wa matofali ya sementi na udongo kwa kila kata | Vikundi 72 vimeundwa<br>Mikutano 75 imeendeshwa<br>Mafunzo yameendeshwa | Idadi ya vikundi vilivyoundwa<br>Kumbukumbu za mkutano na karatasi za mahudhurio<br>Ripoti ya mafunzo | DO II<br>TECH |
